**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM**

# SERA YA TAIFA YA WAZEE YA MWAKA 2003, TOLEO LA MWAKA 2024

**OKTOBA, 2024**

## YALIYOMO


**DIBAJI** ........................................ iv
**TAFSIRI YA MANENO** ........................................ vii
**VIFUPISHO** ........................................ ix
**SURA YA KWANZA** ........................................ 1
**1.1 Utangulizi** ........................................ 1
**1.2 Hali ilivyo ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mwaka 2003** ........................................ 3
1.2.1 Utekelezaji wa Masuala ya Kisera ya Sera ya Taifa ya Wazee 2003 ........................................ 4
1.2.2 Muhtasari wa Yaliyojitokeza kwenye Hali Ilivyo ya Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mwaka 2003 ........................................ 21
1.2.2.1 Mafanikio ........................................ 21
1.2.2.2 Upungufu ........................................ 22
1.2.2.3 Changamoto ........................................ 23
1.2.3 Maeneo Ambayo Hayakujumuishwa Kwenye Sera ya Wazee (2003) ........................................ 24
1.2.3.1 Miundombinu na Mazingira Wezeshi kwa Wazee ........................................ 24
1.2.3.2 Wazee na Teknolojia ........................................ 26
1.2.3.3 Huduma za Afya ya Akili na Msaada wa Kisaikolojia na Kijamii ........................................ 27
1.2.3.4 Masuala Mtambuka ya Sera ........................................ 28
**SURA YA PILI** ........................................ 30
**UMUHIMU WA SERA, DIRA, DHIMA NA MALENGO** ........................................ 30
2.1 Umuhimu wa Sera ........................................ 30
2.2 Dira, Dhima na Malengo ya Sera ........................................ 30
**2.2.1 Dira** ........................................ 30
**2.2.2 Dhima** ........................................ 31
**2.2.3 Malengo ya Sera** ........................................ 31
**SURA YA TATU** ........................................ 33
**HOJA NA MATAMKO YA SERA** ........................................ 33
3.1 Utangulizi ........................................ 33
3.2 Masuala ya Kisera ........................................ 34
3.2.1 Huduma za Afya kwa Wazee ........................................ 34
3.2.2 Matunzo Kwa Wazee ........................................ 35
3.2.3 Ulinzi na Usalama wa Wazee ........................................ 36
3.2.4 Umuhimu wa Jamii Kujiandaa Kabla ya Kufikia Uzee ........................................ 37
3.2.5 Ujasiriamali Jamii kwa Wazee ........................................ 37
3.2.6 Wazee na Teknolojia ........................................ 39
3.2.7 Huduma za Afya ya Akili na Msaada wa Kisaikolojia na Kijamii ........................................ 39

3.2.8 Ushirikishwaji wa Wazee katika Mipango ya Maendeleo na Masuala na Masuala ya Kijamii ........ 41
3.2.9 Miundombinu na Mazingira Wezeshi kwa Wazee ........ 42
3.2.10 Masuala Mtambuka ya Sera ........ 43
**SURA YA NNE** ........ 47
**MUUNDO WA KISHERIA** ........ 47
**SURA YA TANO** ........ 49
**MUUNDO WA KITAASISI** ........ 49
5.1 Utangulizi ........ 49
5.2 Majukumu ya wadau ........ 49
5.2.1 Wizara yenye Dhamana ya Ustawi na Maendeleo ya Wazee ........ 50
5.2.2 Wizara yenye Dhamana ya Masuala ya Afya ........ 50
5.2.3 Wizara yenye Dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ........ 51
5.2.4 Sekretarieti za Mikoa ........ 51
5.2.5 Mamlaka za Serikali za Mitaa ........ 52
5.2.6 Wizara yenye Dhamana ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ........ 53
5.2.7 Wizara yenye Dhamana ya Usalama wa Raia ........ 53
5.2.8 Wizara yenye Dhamana ya Fedha ........ 53
5.2.9 Wizara yenye Dhamana ya Masuala ya Mipango ........ 54
5.2.10 Wizara yenye Dhamana ya Masuala ya Hifadhi ya Jamii ........ 54
5.2.11 Wizara yenye Dhamana ya Masuala ya Ujenzi wa Miundombinu ........ 54
5.2.12 Wizara yenye Dhamana ya Masuala ya Katiba na Sheria ........ 54
5.2.13 Wizara yenye Dhamana ya Masuala ya Kilimo ........ 54
5.2.14 Wizara yenye Dhamana ya Mifugo na Uvuvi ........ 55
5.2.15 Wizara yenye Dhamana ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ........ 55
5.2.16 Wizara yenye Dhamana ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari 55
5.2.17 Wizara yenye Dhamana ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ........ 55
5.2.18 Wizara yenye Dhamana ya Ujenzi ........ 55
5.2.19 Wizara yenye Dhamana ya Viwanda na Biashara ........ 56
5.2.20 Wizara yenye Dhamana ya Utumishi na Utawala Bora ........ 56
5.2.21 Wadau wa Maendeleo ........ 56
5.2.22 Asasi za Kiraia ........ 56
5.2.23 Sekta Binafsi na Taasisi za Dini ........ 56
5.2.24 Taasisi za Elimu na Tafiti ........ 57

5.2.25 Vyombo vya Habari ..... 57
5.2.26 Mabaraza ya Wazee ..... 57
5.2.27 Familia na Jamii ..... 58
5.3 Ufuatiliaji na Tathmini ..... 58
5.4 Hitimisho ..... 59

# DIBAJI

Wazee ni mojawapo ya makundi maalum nchini ambayo Serikali imeweka dhamira na msukumo kuhakikisha upatikanaji wa haki zao na kuboreshwa kwa ustawi na maendeleo yao. Sera ya Taifa ya Wazee ya Mwaka 2003 ni mwongozo muhimu katika kuhakikisha wazee wanapata huduma bora za maisha. Sera hiyo imeainisha maeneo 15 ya kuboresha hali ya maisha ya wazee ambayo ni: Huduma za Afya; Matunzo ya Wazee; Ushirikishwaji wa Wazee; Mfuko wa Wazee; Uzalishaji Mali; Hifadhi ya Jamii; Mahitaji ya Msingi ya Maisha ya Uzeeni; Elimu; Wanawake Wazee na Mila Zilizopitwa na Wakati; Sheria Zisizolinda na Kuendeleza Maslahi ya Wazee; Wanawake Wazee Wenye Ulemavu; Malezi na Maandalizi ya Vijana Kuelekea Uzeeni; Vyama vya Kuhudumia Wazee; Mabaraza ya Wazee; na Ushirikishwaji wa Wadau.

Taarifa ya Tathmini ya mwaka 2023 ya Sera ya Taifa ya Wazee ya Mwaka 2003, imeonesha mafanikio mbalimbali ambayo ni pamoja na: Kuimarika kwa utaratibu unaowawezesha wazee kupewa kipaumbele cha kutibiwa kwanza wanapofika katika vituo vya kutolea huduma za afya vya umma kwa kuhakikisha uwepo wa madirisha ya kuwahudumia; Kuwezesha matunzo ya wazee katika makazi ya wazee na wasiojiweza; Kupungua kwa mauaji ya wazee na kuongezeka kwa ushiriki wa wazee katika shughuli za maendeleo. Aidha, changamoto zilizobainika ni pamoja na: Kukosekana kwa huduma jumuishi za kiafya na wataalam bobezi na wenye ubingwa (*geriatrician*) mahsusi kwa wazee na kuendelea kuwepo kwa maradhi yanayotokana na mtindo wa maisha ikiwemo maisha bwete na ulaji unaosababisha madhara uzeeni; Matunzo duni kwa wazee katika ngazi ya familia na jamii yanayosabishwa na umaskini na vitendo vya utelekezaji kwa wazee; Kuendelea kuwepo kwa vitendo vya ukatili vinavyosababishwa na mila na imani potofu zinazoendeleza kuwepo kwa utelekezaji, ubaguzi, unyanyasaji na mauaji dhidi ya wazee; Uchangiaji mdogo katika mifuko ya hifadhi ya jamii unaosababishwa na uelewa mdogo wa jamii kuhusu umuhimu wa kuweka akiba ya uzeeni; Kukosekana kwa mifumo ya maandalizi ya jamii kuanzia utotoni hadi kufikia maisha ya uzeeni; Ushiriki mdogo wa wazee katika kutumia ujuzi na uzoefu wao katika shughuli za ujasiriamali jamii; Wazee kutokuendana na mabadiliko ya kukua kwa

teknolojia; Kutozingatiwa kwa ujenzi wa miundombinu wezeshi kwa wazee kwenye majengo na makazi binafsi; na Kuendelea kuwepo kwa mila na desturi potofu.

Taarifa ya Tathmini ya Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Wazee ya 2003 vilevile imebaini kujitokeza kwa maeneo yenye upungufu wa kisera unaokwamisha uboreshaji wa huduma za ustawi kwa wazee. Maeneo hayo ni pamoja na: Kukosekana kwa matamko mahsusi ya kushughulikia eneo la miundombinu rafiki na mazingira wezeshi kwa wazee ili kufikia huduma stahiki na kwa wakati; Kukosekana kwa eneo linatoa maelezo juu ya huduma za afya ya akili na msaada wa kisaikolojia kwa wazee; Kutokujumuishwa kwa eneo la teknolojia ambalo litarahisisha shughuli mbalimbali za wazee; Kutojumuishwa kwa wanaume wazee kama kundi linaloathiriwa na mila, imani na desturi potofu; Sera kutojumuisha kundi la wanaume wazee wenye ulemavu; Sera kutojumuisha makundirika yote katika kujiandaa na maisha ya uzeeni; Kutokuwa na masuala mtambuka; na Kutojumuishwa kwa mipango mipya ya maendeleo ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa iliyoandaliwa baada ya Sera hii kutungwa katika maeneo ya teknolojia mpya, ushiriki wa wazee katika vyombo vya maamuzi, ufikiaji wa huduma rafiki na upatikanaji wa huduma za kifedha ikiwemo mikopo. Mipango hiyo ni pamoja na: Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025); Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu (2011/12 – 2025/26); Agenda ya Maendeleo ya Afrika (2063); na Malengo ya Maendeleo Endelevu (2030). Maeneo hayo ni msingi wa kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Wazee ya Mwaka 2003.

Sera ya Taifa ya Wazee ya Mwaka 2003, Toleo la Mwaka 2024, inalenga kuimarisha upatikanaji wa huduma za matunzo, ustawi na ulinzi kwa wazee katika familia, jamii na taasisi mbalimbali. Utekelezaji wa Sera hii utajikita katika maeneo 12. Vilevile, Sera imeweka msisitizo na msingi imara katika kutatua changamoto na upungufu uliobainishwa kwa kuainisha mikakati mbalimbali ya kukabiliana nazo.

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wataalam wa Wizara na wadau wote waliochangia na kuwezesha kukamilika kwa Sera ya Taifa ya Wazee ya Mwaka 2003 Toleo la Mwaka 2024. Aidha, Wizara itashirikiana

na wadau wote ili kuhakikisha Sera hii inatekelezwa kwa maslahi na ustawi wa wazee hapa nchini.

***Dkt.*** Dorothy Gwajima (Mb.)

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM**

## TAFSIRI YA MANENO

Kwa madhumuni ya Sera hii, maneno yafuatayo yatakuwa yanamaanisha kama ifuatavyo: -

| | |
|---|---|
| Mzee | Ni mtu yeyote mwenye umri wa miaka 60 na kuendelea. |
| Ndugu | Mtu mwenye uhusiano wa kuzaliwa, ndoa na kuasili. |
| Mzee Asiyejiweza | Ni mtu mwenye umri wa miaka 60 na kuendelea ambaye amepungukiwa uwezo wa kufanya kazi, asiye na ndugu wala jamaa wa kumtunza au aliyetelekezwa bila msaada wowote. |
| Matunzo | Huduma muhimu kwa wazee wanaoishi katika familia/jamii na Makazi ya Wazee. |
| Makazi ya Wazee<br><br>Wasiojiweza | Jengo au nyumba zilizoandaliwa mahsusi kwa ajili ya kuwapatia wazee na wasiojiweza hifadhi, matunzo na ulinzi. |
| Uzee na Kuzeeka | Ni dhana inayoelezea hatua ya makuzi ya binadamu kuanzia utoto, ujana hadi kufikia uzee. |
| Ulemavu | Ni hali inayotokana na dosari mwilini au/akilini ambayo inasababisha mtu kushindwa kutenda mambo ambayo kwa kawaida angetegemewa kuyaweza na hivyo kumletea mtu huyo kizuizi katika utekelezaji wa majukumu yake katika jamii. Kizuizi katika utendaji kinatokana pia na mfumo wa mtazamo wa jamii dhidi ya mtu huyo. |

| | |
|---|---|
| Hifadhi ya Jamii | Ni kinga/kitendo cha ulinzi kinachotolewa kwa jamii na wanajumuiya wake kupitia misaada mbalimbali dhidi ya dhiki ya kiuchumi na kijamii ambayo inaweza kusababishwa na uzee, kifo, ulemavu na kupungua kwa mapato kutokana na sababu mbalimbali. |

| VIFUPISHO | |
|---|---|
| AIDS | Acquired immunodeficiency syndrome |
| HIV | Human immunodeficiency virus |
| NCDs | Non-Communicable Deseases |
| NSSF | National Social Security Fund |
| PPRA | Public Procument Regulatory Authority |
| PSSSF | Public Service Social Security Fund |
| SACCOS | Savings and Credit Cooperative Societies |
| SADC | Sourthen African Development Community |
| TASAF | Tanzania Social Action Fund |
| TCRA | Tanzania Communication Regulating Authority |
| UKIMWI | Upungufu wa Kinga Mwilini |
| VICOBA | Village Community Bank |
| VVU | Virusi vya UKIMWI |

# SURA YA KWANZA

## 1.1 Utangulizi

Uzee na kuzeeka ni dhana inayoelezea hatua ya makuzi ya binadamu kuanzia utoto, ujana hadi kufikia uzee. Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, Tanzania ilikuwa na jumla ya watu 61,741,120. Katia yao, Tanzania bara ilikuwa na jumla ya Wazee 3,406,464 (Me 1,546,221 na Ke 1,860,243) ikilinganishwa na Sensa ya Watu ya Mwaka 2012 ambapo idadi ya watu ilikuwa 44,928,923 na kati yao wazee walikuwa 2,507,568 (Me 1,200,210 na Ke 1,307,358).

Tangu Uhuru Serikali imekuwa ikiweka mikakati na mipango ya kuwahudumia wazee hapa nchini. Azimio la Arusha la Mwaka 1967 liliainisha wazee, watoto na watu wenye ulemavu kama makundi ambayo yanapaswa kupewa msukumo maalum katika kupata matunzo, ulinzi na msaada kutoka kwa jamii. Serikali iliridhia Mpango Kazi wa Umoja wa Mataifa wa Vienna wa Mwaka 1982 ambao uliweka dira ya utoaji wa huduma na ushirikishwaji wa wazee katika shughuli za maendeleo. Mpango huu ulifanyiwa mapitio mwaka 2002 kwa lengo la kuainisha changamoto na mahitaji ya wazee katika karne ya 21. Aidha, mwaka 1999 katika kuadhimisha Mwaka wa Kimataifa wa Wazee, Serikali ilifanya uamuzi wa kuwa na Sera mahsusi ya wazee ambapo mwaka 2003 Sera ya Taifa ya Wazee ilitungwa.

Lengo kuu la Sera ya Taifa ya Wazee ya mwaka 2003 lilikuwa ni kuhakikisha kuwa wazee wa Tanzania wanatambuliwa na kupewa fursa ya kushiriki katika mambo yanayohusu maisha ya kila siku kwa manufaa ya Watanzania wote. Pia kuhakikisha kwamba wazee wanapata huduma zote

muhimu na za msingi ambazo zitawawezesha kushiriki kikamilifu katika maisha ya kila siku.

Malengo mahsusi ya Sera yalikuwa ni: Kutoa nafasi kwa wazee ili watambulike kuwa ni rasilimali badala ya kuonekana ni mzigo kwa familia na jamii; Kujenga mazingira ya kumwezesha mzee kupata na kutumia huduma muhimu za kijamii ili aweze kuishi kwa usalama na heshima; Kutenga rasilimali za kutosha kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na ustawi wa wazee kwa kuzingatia haki, wajibu na majukumu yao; Kuwezesha na kuchochea uzalishaji mali katika familia ili ziweze kutoa huduma za msingi kwa wazee; Kuanzisha na kuendeleza programu zinazotoa fursa kwa wazee kushiriki katika mipango ya kiuchumi kwa ajili ya maendeleo yao; Kuandaa mikakati na programu zinazolenga katika utoaji wa picha nzuri ya wazee na kupiga vita mawazo potofu yanayoambatana na ubaguzi kiumri; Kutunga sheria ambazo zitalinda na kuendeleza ustawi wa wazee; Kuhakikisha kuwa wazee wanapata huduma za afya ya msingi; Kuanzisha na kuendeleza programu zinazoelimisha vijana kuhusu masuala ya uzee na kuzeeka na kuwajengea uwezo wa kufanya maandalizi ya maisha kuelekea uzeeni; na Kuandaa programu zitakazotoa fursa kwa wazee kuendeleza mila, desturi na maadili mema kwa vijana katika jamii.

Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Wazee ya Mwaka 2003 ulijikita katika maeneo makuu 15 ambayo ni: Huduma za Afya; Matunzo ya Wazee; Ushirikishwaji wa Wazee; Mfuko wa Wazee; Uzalishaji Mali; Hifadhi ya Jamii; Mahitaji ya msingi ya maisha uzeeni; Elimu; Wanawake wazee na mila zilizopitwa na wakati; Wanawake wazee wenye ulemavu; Sheria zisizolinda na kuendeleza maslahi ya wazee; Malezi na maandalizi ya

vijana kuelekea uzeeni; Vyama vya kuhudumia wazee; Mabaraza ya Wazee; na Ushirikishwaji wa wadau.

Kutokana na changamoto na upungufu wa kisera uliojitokeza, Tathmini ya Utekelezaji wa Sera iliyofanyika mwaka 2023 imeonesha umuhimu wa kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Wazee ya Mwaka 2003 ili kutatua upungufu na changamoto hizo. Vilevile, tathmini imebaini umuhimu wa kuendelea na maeneo yaliyoonesha mafanikio ambayo katika Sera hii yatashughulikiwa kwa mtazamo tofauti unaoendana na mazingira ya sasa. Lengo likiwa ni kuimarisha upatikanaji wa huduma za matunzo, ustawi na ulinzi kwa wazee katika jamii na taasisi mbalimbali.

Umuhimu wa kufanya mapitio ya Sera hii pia umetokana na kuwepo kwa baadhi ya mipango ya kimataifa, kikanda na kimataifa kama vile Agenda ya Maendeleo ya Afrika (2063) inayosisitiza ushiriki wa watu wote kwenye ngazi za uamuzi na Malengo ya Maendeleo Endelevu (2030) inayosisitiza pamoja na mambo mengine uwepo wa usawa katika jamii na kuinua hali ya maisha ya makundi maalum wakiwemo wazee katika matumizi ya teknolojia mpya na upatikanaji wa huduma rafiki za kifedha na huduma muhimu kwa wazee.

## 1.2 Hali ilivyo ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mwaka 2003

Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Wazee ya Mwaka 2003 umeonesha mafanikio makubwa katika kuleta ustawi na maendeleo ya wazee. Mafanikio haya yametokana na ushirikiano kati ya Serikali na wadau mbalimbali wakiwemo Washirika wa Maendeleo, Sekta binafsi, Asasi za Kiraia na jamii kwa ujumla. Hivyo, kipengele hiki kina lengo la kubainisha hali halisi ya jitihada za kuwezesha ustawi na maendeleo ya wazee, mafanikio na changamoto.

### 1.2.1 Utekelezaji wa Masuala ya Kisera ya Sera ya Taifa ya Wazee 2003

Tathmini ya utekelezaji imezingatia maeneo ya msingi katika Sera ya Taifa ya Wazee ya mwaka 2003 kama ifuatavyo:

#### 1.2.1.1 Huduma za Afya

Sera ya Taifa ya Wazee (2003) inatambua wazee kama kundi maalum lililo katika hatari zaidi ya kuathiriwa na magonjwa mbalimbali ikilinganishwa na makundi mengine. Aidha, Sera hii ilibainisha umuhimu wa kuhakikisha Sera ya Taifa ya Afya ya Mwaka 2007 inafanyiwa mapitio kwa lengo la kurekebisha vigezo vya utambuzi wa umri wa miaka 60; watumishi wa afya kupewa mafunzo maalum ya namna ya kuwahudumia wazee; kuweka utaratibu wa kufuatilia afya za wazee katika jamii; kuweka utaratibu wa kuhamasisha na kushauri wazee kuhusu tatizo la VVU na UKIMWI, matunzo ya wazee waliyoathirika na wananchi kwa ujumla wanahamasishwa kuhusu matatizo ya kiafya yanayotokana na uzee kupitia njia mbalimbali.

Vilevile, Tathmini ilibainisha kuwa Sera ya Taifa ya Afya iliandaliwa na kuzingatia makundi maalum likiwemo kundi la wazee wasiojiweza kutokuchangia gharama za matibabu. Aidha, mafanikio ya Sera hii ni pamoja na kuwatambua na kuwapatia vitambulisho vya matibabu. Kuanzia mwaka 2015 hadi kufikia Juni 2023, jumla ya wazee 2,203,414 (Me 1,005,076 na Ke 1,198,338) wametambuliwa, kati ya hao wazee wasio na uwezo 1,256,544 wamepatiwa vitambulisho vya matibabu bila malipo. Aidha, kupitia Kampeni ya “Mpishe Mzee Kwanza”, vituo vyote vya kutolea huduma za afya vya Serikali vinatoa kipaumbele kwa wazee kupata huduma za afya. Pia, Serikali imeelekeza kutengwa kwa dirisha maalum kwa ajili ya wazee kwenye hospitali na vituo vya afya vya umma ambapo

hadi kufikia Juni, 2023 jumla ya madirisha 629 ya kutolea huduma kwa wazee yametengwa katika hospitali na vituo vya umma vya kutolea huduma za afya kote nchini.

Tathmini ilibainisha pia kuwa, pamoja na kutolewa kwa mafunzo maalum kwa watumishi wa afya kwa ajili ya kuwahudumia wazee, bado kumekuwepo na uhaba mkubwa wa wataalamu hao hapa nchini. Hali hii inaonesha ni kwa kiasi gani nchi inahitaji kuweka msukumo mkubwa wa kuhamasisha upatikanaji wa wataalam hao hasa ikizingatiwa kuwa uhitaji kwa wazee umeongezeka.

Katika kuhakikisha kuwa jamii inawekewa utaratibu wa kufuatilia afya za wazee, Tathmini ilibaini kuwa Serikali imeweka utaratibu wa kuelimisha jamii juu ya afya zao kupitia klabu za wazee, ambapo hadi kufikia mwaka 2023, jumla ya klabu 263 zimeanzishwa nchini. Aidha, Serikali imeendelea kutoa elimu na uhamasishaji juu ya magonjwa yasiyoambukiza na yanayoambukiza kupitia njia mbalimbali ikiwemo vyombo vya habari, semina, makongamano na maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wazee ambapo wazee hujitokeza kupima afya zao na kupata taarifa mbalimbali kuhusu namna ya kujikinga na maradhi. Katika kipindi cha mwaka 2022, jumla ya wazee 19,411 walipimwa afya zao na kupatiwa huduma za matibabu kwenye Maadhimisho ya Kimataifa ya Siku ya Wazee. Pamoja na uelimishaji kupitia maadhimisho, upo umuhimu wa kuweka mifumo ya kuhakikisha kuwa wazee na jamii inayowatunza wanapata ufahamu juu ya umuhimu wa kufuatilia afya zao na kuchukua hatua stahiki.

Serikali imeendelea kuielimisha jamii kuhusu umuhimu wa kuwatunza wazee na kuhakikisha upatikanaji wa haki, ustawi na maendeleo yao. Katika kuimarisha huduma za afya kwa wazee, Serikali imeendelea

kuratibu upatikanaji wa huduma bora za afya bila malipo kwenye vituo vyote vya kutolea huduma za afya vya umma hususan kwa wazee wasio na uwezo. Serikali ilianzisha utaratibu wa kuwatambua wazee, kutathmini hali zao na kutoa vitambulisho vya matibabu bila malipo kwa wazee wasiojiweza. Hii ni kutokana na hali duni ya maisha inayowakabili wazee hususan wale wanaoishi vijijini kushindwa kugharamia matibabu yao. Kutokana na hali hii, Sera iliweka malengo ya kuboresha huduma za afya kwa wazee kwa kufanya mapitio ya taratibu za uchangiaji wa huduma za afya na kutoa mafunzo maalum kwa watoa huduma za afya kuhusu namna ya kuwahudumia wazee na kuhamasisha wazee na jamii kwa ujumla kuhusu kukabiliana na matatizo ya kiafya yanayotokana na uzee.

Taarifa ya Tathmini ya Utekelezaji wa Sera imebaini kukosekana kwa huduma za afya jumuishi zinazosababishwa na kukosekana kwa wataalam bobezi na wenye ubingwa mahsusi kwa wazee (geriatrician) na kuendelea kuwepo kwa maradhi yanayotokana na mtindo wa maisha ikiwemo maisha bwete na ulaji unaosababisha madhara uzeeni.

#### 1.2.1.2 Matunzo ya Wazee

Sera ya Taifa ya Wazee ya Mwaka 2003 imebainisha kuwa suala la matunzo kwa wazee katika jamii ni jukumu la familia, jamii na ndugu wa karibu. Aidha, suala la kutoa matunzo kwa wazee katika makazi ni hatua ya mwisho, endapo itabainika kuwa mzee husika hana ndugu wa kumtunza katika jamii. Katika kipindi cha mwaka 2015 - 2022, jumla ya wazee 2,135 wamepata hifadhi katika makazi yote ya wazee nchini. Kiwango hiki kinadhihirisha kuwa Serikali imeimarisha huduma ya matunzo kwa wazee katika jamii kupitia utekelezaji wa mipango na programu mbalimbali. Kupitia maadhimisho mbalimbali ikiwemo Siku ya Kimataifa ya Wazee, mabaraza

ya ushauri ya wazee na mashirika ya kuhudumia wazee, Serikali inahamasisha na kuelimisha jamii kutekeleza wajibu wao wa kuhudumia makundi maalum katika jamii wakiwemo wazee. Aidha, kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), huduma za matunzo kwa wazee zimeimarika kutokana Mfuko huu kupitia ruzuku inayotolewa katika ngazi ya kaya kuwawezesha wazee kumudu kupata mahitaji ya msingi. Hadi kufikia Machi, 2022 jumla ya wazee 525,658 walinufaika na mpango huo.

Vilevile, katika kuimarisha matunzo kwa wazee wasiojiweza, huduma katika makazi ya wazee zimeendelea kutolewa ambapo Serikali imetekeleza mpango wa kuunganisha Makazi ya wazee uliolenga kupunguza makazi kutoka makazi 17 hadi makazi 13. Wahudumiwa wa makazi yaliyofungwa walitengamanishwa katika jamii na baadhi yao kuhamishiwa katika makazi mengine yanayoendeshwa na Serikali. Mpango huu umelenga kuboresha huduma na miundombinu katika makazi hayo. Katika kipindi cha mwaka 2015 hadi 2023, wastani wa wazee 270 wamekuwa wakipatiwa huduma za chakula, malazi, mavazi, huduma za afya, msaada wa kisaikolojia na huduma za kiroho kila mwaka. Serikali pia inasimamia utoaji wa huduma kwa wazee katika makazi 15 yanayoendeshwa na taasisi binafsi na mashirika ya dini yenye jumla ya wahudumiwa 268 (Me 118 na Ke 150). Vilevile, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu kwa kufanya ukarabati wa majengo, mifumo ya umeme na maji katika makazi ya wazee ya Misufini (Tanga), Nunge (Dar es Salaam), Kolandoto (Shinyanga), Njoro (Kilimanjaro), Magugu (Manyara) na Sukamahela (Singida), Fungafunga (Morogoro) na Ipuli (Tabora).

Pamoja na mafanikio ya utekelezaji katika eneo la matunzo kwa wazee, changamoto iliyojitokeza ni kutokuwepo kwa mfumo maalum wa usimamizi na kuhakikisha familia ikiwemo watoto wanatoa huduma stahiki za matunzo kwa wazee wao. Mabadiliko ya kijamii na kiuchumi yamesababisha kuzorota kwa hali ya matunzo hususan kwa wazee wanaoishi vijijini. Hali hii kwa kiwango kikubwa inatokana na kukua kwa miji ambayo imesababisha vijana kukimbilia mijini na kuwaacha wazee bila msaada wowote. Pamoja na hali ngumu ya maisha inayowakabili wazee, pia wazee wamechukua jukumu la matunzo ya wajukuu baada ya wazazi wao kufariki au kutelekezewa watoto wakati wazazi wao wakitafuta fursa za kiuchumi mijini. Suala hili linaweza kusababisha watoto hao waliotelekezwa kutotambua thamani na mchango wa wazazi wao hali itakayoathiri matunzo ya wazazi hao wakati wa uzee.

Aidha, hali duni ya matunzo kwa wazee imesababishwa na kudhoofika kwa mifumo ya asili ya malezi, matunzo na ulinzi kwa wazee ambapo familia na jamii nyingi zimesahau wajibu wao wa msingi wa kuwatunza wazee na kusababisha wazee kuishi maisha duni.

#### 1.2.1.3 Wanawake Wazee na Mila Zilizopitwa na Wakati

Sera ya Taifa ya Wazee ya mwaka 2003 imeelekeza kutoa elimu kwa jamii kuhusu mila na desturi zilizopitwa na wakati ili kuwezesha usawa katika jamii. Aidha, Sera hii imelenga kuimarisha ulinzi kwa wazee hususan wanawake ili kuwalinda dhidi ya vitendo vya ukatili ikiwemo mauaji ambayo kwa kiwango kikubwa yanatokana na kuwepo kwa mila zenye madhara.

Katika kukabiliana na mila zenye madhara, Serikali kwa kushirikiana na wadau imetekeleza afua mbalimbali za kusaidia jamii kuachana na mila hizo. Hatua mojawapo ni kuandaa na kutekeleza Mpango Kazi wa Taifa wa

Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) wa mwaka 2017/18 – 2021/22 ambao umeweka eneo mahsusi la kushughulikia mila na desturi kandamizi kwa wanawake wakiwemo wazee**.** Mpango huu umesaidia kuwepo kwa mifumo shirikishi ya ulinzi katika ngazi ya jamii ambayo ni mahsusi katika kuzuia vitendo vya ukatili kupitia afua mbalimbali na kusimamia utoaji wa huduma kwa wahanga. Kupitia utekelezaji wa Mpango Kazi huu hadi kufikia Juni 2023, jumla ya kamati za ulinzi wa wanawake na watoto 18,186 zilikuwa zimeundwa kuanzia ngazi ya Taifa hadi kijiji/mtaa. Sambamba na Mpango Kazi huo, Serikali inaratibu utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Kutokomeza Mauaji ya Wazee (2018/19 – 2022/23), na MTAKUWWA II wa Mwaka 2024/25 – 2028/29. Mkakati huu unalenga kutokomeza mauaji ya wazee na kuhakikisha wazee wanatambuliwa na kulindwa dhidi ya ubaguzi, uonevu, unyanyasaji na ukatili unaotokana na mila zenye madhara. Kwa mujibu wa taarifa kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2021 hapakuwa na matukio ya mauaji kwa wazee. Hata hivyo, kwa mujibu wa taarifa ya Wizara hiyo katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2022 matukio ya mauaji yaliyoripotiwa yalikuwa 130, (me 29, ke 101).

Vilevile, Serikali imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu kutokomeza mila zenye madhara ambazo huchangia katika ukatili kwa wazee hususan wanawake kupitia maadhimisho mbalimbali. Katika kipindi cha 2015 hadi 2023, jumla ya washiriki 25,441 walipatiwa elimu hiyo kupitia maadhimisho ya Siku ya Wazee Duniani ambayo huadhimishwa tarehe 1 Oktoba kila mwaka na Maadhimisho ya Siku ya Kupinga Ukatili Dhidi ya Wazee ambayo huadhimishwa tarehe 15 Juni kila mwaka.

Kutokana na kuwepo kwa mila zinazokandamiza wanawake hususan katika masuala ya umiliki wa ardhi, Serikali kupitia Mpango wa Umiliki Ardhi wa Mwaka 2014 - 2017 iliwezesha kuongezeka kwa wanawake wanaomiliki ardhi kutoka asilimia 9 hadi asilimia 25. Aidha, umiliki wa pamoja baina ya wanandoa umeongezeka kutoka asilimia 6 hadi asilimia 16 (*Land Tenure Support Program Evaluation Report, 2017*). Vilevile, Serikali imetunga Sheria ya Msaada wa Kisheria Sura ya 21 na Kanuni za Mahakama na Matumizi ya Sheria (Mwenendo wa Mashauri yanayohusisha Makundi ya Walio katika Mazingira Hatarishi za Mwaka 2019) ambayo inasaidia pia makundi maalum wakiwemo wazee kupata msaada wa kisheria kupitia watoa msaada wa kisheria ambao wanaratibiwa na Serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria.

Serikali pia imeendelea kuwasajili watoa huduma za msaada wa kisheria katika mikoa yote hapa nchini ili kutoa huduma za msaada wa kisheria kwa makundi maalum na watu wenye shida mbalimbali na wasio na uwezo wakiwemo wazee. Hadi mwezi Juni 2023, jumla ya taasisi 225 zinazotoa msaada wa kisheria zimesajiliwa na jumla ya watoa msaada wa kisheria 1,495 wamesajiliwa ambao wanatoa huduma za msaada wa kisheria kwa watu wasio na uwezo wa kumwajiri wakili. Vilevile, Serikali kupitia Jeshi la Polisi inaendelea kuunda Madawati ya Jinsia na Watoto ambapo hadi kufikia Desemba 2022, jumla ya madawati 420 yameundwa katika vituo vya Polisi nchini. Kupitia madawati haya, makundi maalum likiwemo la wazee hupata huduma za msaada wa kisheria.

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Sera hii, bado kumekuwepo na changamoto mbalimbali zinazowakabili wanawake wazee vikiwemo vitendo vya ukatili na unyanyasaji kwa wazee hususan mauaji ya

wazee kutokana na sababu mbalimbali za imani za kishirikina na kutofikiwa na huduma za msaada wa kisheria. Aidha, pamoja na kwamba Sera hiyo ililenga zaidi kushughulikia mila zilizopitwa na wakati kwenye kundi la wanawake wazee, mila hizi pia ziliathiri kundi la wanaume wazee.

Tathmini imebaini suala la wanawake wazee na mila zilizopitwa na wakati bado limeendelea kuwepo, hivyo kutokana na changamoto zingine zinazohusisha maeneo mengine zaidi ya mila ikiwemo imani na desturi zinazoathiri ulinzi na usalama kwa wazee wa kike na kiume. Hivyo katika sera hii, eneo hili litashughulikiwa kwa mtazamo wa ulinzi na usalama kwa wazee.

#### 1.2.1.4 Sheria Zisizolinda na Kuendeleza Maslahi ya Wazee

Sera ya Taifa ya Wazee (2003) inatamka kuhusu kutungwa kwa sheria mahsusi itakayolinda na kuboresha maisha ya wazee. Umuhimu wa sheria hiyo ulikuwa ni kulinda na kuwaendeleza wazee na maisha yao. Umuhimu huo umeendelea kubainika na kuhakikisha kuwa afua mbalimbali kwa wazee zinatekelezwa na kuwekewa usimamizi na udhibiti wa shughuli na huduma zinazotolewa kwa ajili ya kulinda haki na ustawi wa wazee. Taarifa ya Tathmini imebainisha kuwa masuala ya wazee yanashughulikiwa na sheria za sekta mbalimbali zikiwemo sheria za ardhi, kodi na hifadhi ya jamii, ambapo imebainishwa kwamba sheria katika sekta hizo zina upungufu ambao huleta changamoto ya ufanisi na utoshelevu wa upatikanaji wa huduma kwa wazee.

#### 1.2.1.5 Mfuko wa Wazee

Sera ya Taifa ya Wazee (2003) inatamka kuwa kutaanzishwa Mfuko wa Wazee (*Revolving Loan Fund*) kwa lengo la kuwawezesha wazee kupata

mikopo nafuu ili kuendesha shughuli za kiuchumi zitakazowasaidia kujikimu kimaisha. Tathmini imebaini kuwa katika utekelezaji wa Sera hii, Serikali haikuweza kuanzisha mfuko maalum kwa ajili ya wazee. Hata hivyo, kwa kushirikiana na wadau imeendelea kuwahamasisha wazee na kuwaunganisha katika programu mbalimbali za kuwezesha wananchi kiuchumi. Vilevile, Taarifa ya Tathmini imebaini kuwa pamoja na kutokuwepo na mfuko huo, wazee wastaafu wameendelea kupata huduma za mikopo yenye masharti nafuu kwa ajili ya kuendesha miradi ya uzalishaji mali ambapo hadi kufikia mwezi Mei 2020, jumla ya wazee wastaafu 49,344 (Me 39,616 na Ke 9,728) walipatiwa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 298.6 kupitia iliyokuwa Benki ya Posta Tanzania.

Aidha, wanawake wazee na wenye ulemavu wana fursa ya kupata mikopo isiyo na riba kupitia mifuko ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo zimekuwa zikitengwa kwa ajili ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kutokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani (asilimia 4 wanawake, asilimia 4 vijana na asilimia 2 watu wenye ulemavu). Pamoja na fursa hiyo ya wanawake kupata mikopo, bado Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290 haitoi fursa kwa wazee wanaume na wasio walemavu kupata mikopo hiyo.

Tathmini imebaini kuwa pamoja na kuwepo kwa mifuko na fursa za mikopo, bado kundi la wazee halijapewa kipaumbele kutokana na mifuko kutokuwa na uhakika wa marejesho na utekelezaji mzuri wa malengo ambayo imekuwa ikisababishwa na dhana iliyojengeka miongoni mwa wanajamii kuwa ukiwa mzee hutarajiwi kufanya kazi za uzalishaji ikilinganishwa na vijana. Vilevile, bado kuna uelewa mdogo wa wananchi na wazee wenyewe kuhusu uwepo na faida za fursa hizo za kiuchumi. Kutokana na

changamoto hizo ikiwemo urejeshwaji wa mikopo, suala hili linapaswa kushughulikiwa kwa kuwawezesha wazee kujihusisha na shughuli ndogondogo za ujasiriamali jamii za kujiongezea kipato ili waweze kuaminika na hivyo kukopesheka.

#### 1.2.1.6 Hifadhi ya Jamii

Hifadhi ya Jamii kwa wazee ni mpango wa kuwawezesha wazee kupata huduma muhimu kutokana na akiba waliyojiwekea baada ya kuishiwa uwezo wa kufanya kazi. Sera ya Taifa ya Wazee ya mwaka 2003 inatambua umuhimu wa kupata hifadhi ya jamii uzeeni ili kuwawezesha kukidhi mahitaji ya msingi na kuzifikia huduma mbalimbali. Aidha, Sera hii ililenga kuweka utaratibu utakaohakikisha kwamba taasisi za hifadhi ya jamii zinaelekeza huduma zake katika sekta isiyo rasmi na kuhakikisha kuwa familia na jamii zinahamasishwa ili kushiriki katika shughuli za uzalishaji na kujiwekea akiba.

Taarifa ya tathmini ilibaini uwepo wa Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii, Sura ya 50 inayotambua sekta zisizo rasmi ambapo wazee waliochangia katika mifuko hiyo wameendelea kunufaika na mifuko ya hifadhi ya Jamii. Hadi kufikia Juni, 2023 Serikali imewezesha jumla ya wazee wastaafu 28,820 kunufaika na huduma za hifadhi ya jamii kutoka katika Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (National Social Security Fund-NSSF). Aidha, kupitia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (Public Service Social Security Fund - PSSSF) Serikali imeendelea kulipa mafao ya muda mrefu, pensheni kwa wastaafu na wategemezi kwa mafao ya mirathi. Kufikia mwezi Juni 2023, Mfuko wa PSSSF ulikuwa na jumla ya wanufaika 247,345 wanaolipwa pensheni ya kila mwezi. Aidha, tathmini

imebaini kuwepo kwa mifumo ya hifadhi ya jamii isiyo rasmi ambapo jamii inachangia familia nyingine wakati wa matukio mbalimbali.

Vilevile, tathmini imebainisha kutokuwepo kwa upatikanaji wa huduma za hifadhi ya jamii katika maeneo ya vijijini na kuwepo kwa uelewa mdogo kwa jamii hususan wamiliki wa sekta binafsi kwa kutokuwaunganisha watumishi wao katika mifuko ya hifadhi ya jamii. Pamoja na huduma hizi kuwepo kwenye maeneo ya mijini bado jamii iliyopo kwenye sekta sizizo rasmi haina uelewa wa kutosha kuhusu umuhimu wa kuchangia kwenye mifuko hiyo. Hali hii inasababisha changamoto ya kutokupata mafao uzeeni.

Pamoja na mafanikio ya utekelezaji wa Sera yaliyopatikana, changamoto nyingine zilizobainika ni:

(i) Kiwango cha kima cha chini cha pensheni kwa wazee waliokuwa katika mifumo rasmi ya ajira kutokidhi mahitaji. Kima cha chini kinachotolewa kwa wazee hakihusishi wazee waliokuwa katika sekta isiyo rasmi;

(ii) Kuendelea kuwepo kwa uelewa mdogo wa jamii kuhusu uchangiaji wa hiari katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF);

(iii) Kukosekana kwa elimu ya masuala ya fedha inayosababisha matumizi yasiyozingatia mahitaji ya mafao ya kustaafu kwa wazee hasa pale wazee wanapolipwa mafao ya mkupuo kabla ya kuanza kupokea malipo ya pensheni ya kila mwezi; na

(iv) Wazee wengi wenye uwezo na nguvu kutokujishughulisha na shughuli za kujiongezea kipato baada ya kustaafu.

#### 1.2.1.7 Mabaraza ya Wazee

Wazee ni miongoni mwa wananchi ambao mchango wao ni muhimu katika maendeleo ya nchi yetu. Sera ya Taifa ya Wazee ya mwaka 2003 imeelekeza kuwekwa kwa utaratibu utakaohakikisha upatikanaji wa

mchango wa wazee kuhusu maisha yao na ya jamii kwa ujumla. Vilevile, Sera imeelekeza kuundwa kwa Mabaraza ya Ushauri ya Wazee kwenye ngazi za vijiji/mitaa, Kata, Halmashauri, Mkoa na Taifa kwa ajili ya kuwezesha ushiriki wa wazee katika mipango ya maendeleo.

Kuhusu utekelezaji wa Sera ya Wazee, Tathmini imebaini kuwa hadi kufikia Juni, 2023, jumla ya mabaraza ya ushauri ya wazee 20,749 yameundwa kuanzia ngazi za vijiji/mitaa, Kata, Halmashauri, Mkoa hadi Taifa. Pamoja na kuundwa kwa mabaraza hayo Taarifa ya Tathmini inaonesha kuwa mabaraza hayo yanakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo za: mabaraza kutokutumika ipasavyo katika masuala mbalimbali ya maendeleo ya kijamii, kwa mfano, kuelimisha jamii juu ya mila na desturi nzuri, mazingira na uzalendo pamoja na kutoa ushauri katika utatuzi wa migogoro/changamoto mbalimbali za kijamii.

Vilevile, Taarifa ilibaini ushirikishwaji mdogo wa wazee katika vyombo mbalimbali vya uamuzi. Hali hii inasababisha baadhi ya ajenda zinazowahusu wazee kutokujadiliwa kutokana na kukosekana kwa uwakilishi wao kwenye vyombo hivyo ikilinganishwa na makundi mengine kama vile wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ambao uwakilishi wao upo katika vyombo mbalimbali vya uamuzi. Uwakilishi huo unahusisha vyombo kama vile Bungeni, kamati mbalimbali za kisheria mfano Kamati za Mazingira, Maji na Afya. Kutoshirikishwa kwa wazee katika ngazi hizo kunachangia kutokuingizwa kwa baadhi ya changamoto za wazee kwenye mipango ya maendeleo.

#### 1.2.1.8 Malezi na Maandalizi ya Vijana Kuelekea Uzeeni

Sera ya Taifa ya Wazee ya Mwaka 2003 inaelekeza Serikali kushirikiana na wadau katika kuelimisha jamii hususan vijana kuhusu nafasi ya wazee

na umuhimu wa kufanya maandalizi ya maisha kuelekea uzeeni. Taarifa ya tathmini imebainisha kuwepo kwa programu za kuwajengea uwezo vijana ili kuwawezesha kuendesha shughuli mbalimbali kwa ajili ya maisha yao ambapo itawasaidia katika maisha ya ujana na kuelekea uzeeni. Aidha, kupitia programu hizo, Serikali imewezesha vijana 6,695 kiuchumi kwa kuwapatia mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 5.9 katika vikundi 957.

Vilevile, Serikali imeweka mazingira wezeshi ya upatikanaji wa mitaji kwa kuboresha vyanzo vya akiba na kuchukua hatua za kuondoa vikwazo ili kuwezesha mabenki kukopesha kikamilifu amana zilizopo kwa gharama nafuu kupitia vikundi vidogo vikiwemo Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (*Savings and Credit Cooperative Societies- SACCOS)* na Vikundi vya Kijamii vya Huduma Ndogo za Fedha (*Village Community Bank – VICOBA)*. Katika kuongeza uwezo wa kuwakopesha vijana kupitia asilimia 10 zinazotengwa na Halmashauri kutokana na mapato yao ya ndani kwa mwaka 2021/2022, jumla ya shilingi bilioni 30.39 zilitengwa na kutolewa, mwaka 2022/2023, shilingi bilioni 12.55 zilitengwa na kutolewa kwa vijana. Programu hizi zimesaidia katika kuwaelimisha vijana na kuwajengea uwezo wa kiuchumi na kujiajiri ikiwa ni sehemu ya maandalizi yao kuelekea uzeeni.

Vilevile, Serikali imeratibu na kusimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini katika kutenga maeneo maalum kwa ajili ya shughuli za kiuchumi za vijana. Hadi kufikia mwaka 2020, jumla ya Halmashauri 111 Tanzania Bara zimetenga maeneo yenye jumla ya ekari 217,882 kwa ajili ya shughuli za kilimo, biashara, ufugaji na huduma kwa vijana ili waweze kujiajiri na kupunguza umaskini wa kipato. Aidha, vijana wahitimu wa Elimu ya Juu wamewezeshwa kupata mikopo na kuunda kampuni za biashara. Hadi

kufikia mwaka 2020, jumla ya kampuni 136 za vijana zimeanzishwa ambapo vikundi/kampuni 76 kati ya hizo zimeunganishwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) kwa ajili ya kupata kipaumbele katika kupewa zabuni za kazi mbalimbali zinazotangazwa na Serikali. Dhumuni la Serikali la kuweka jitihada hizi ni kutoa umuhimu kwa vijana kuboresha maisha ya sasa na kuweka mazingira ya kujiandaa kwa ajili ya maisha ya baadaye hivyo kupunguza hali ya utegemezi uzeeni.

Pamoja na mafanikio ya utekelezaji wa tamko hili, miongoni mwa changamoto zilizojitokeza ni:

(i) Kukosekana programu mahsusi zinazowezesha rika zote katika jamii kujiandaa na maisha ya uzeeni; na

(ii) Uelewa mdogo wa vijana kuhusu umuhimu wa kuwekeza na kutumia fursa ili kujiandaa na maisha ya kuelekea uzeeni.

Sera hii ililenga kuwaandaa vijana kuelekea uzeeni, hata hivyo maisha ya uzeeni yanatakiwa kuandaliwa tangu miaka ya awali ya mtoto na kupitia hatua zote za ukuaji anapoelekea uzeeni. Hivyo, jamii yote inatakiwa kuandaliwa katika mtazamo huu.

#### 1.2.1.9 Wanawake Wazee Wenye Ulemavu

Sera ya Taifa ya Wazee ya mwaka 2003 imeelekeza Serikali kuweka utaratibu wa kuwatambua na kuwapa mahitaji ya msingi wanawake wazee wenye ulemavu ikiwemo kuwajumuisha kwenye miradi ya uzalishaji mali kwenye maeneo waliopo.

Katika kutekeleza tamko hilo, Serikali imechukua hatua mbalimbali za kuwawezesha watu wenye ulemavu kiuchumi wakiwemo wanawake wazee. Hii ni pamoja na kutungwa kwa Sheria ya Watu Wenye Ulemavu,

Sura ya 183 inayokataza watu kubaguliwa katika masuala ya ajira kwa misingi ya ulemavu, kila mwajiri mwenye waajiriwa zaidi ya 20 anapaswa kuwa na watu wenye ulemavu wasiopungua asilimia 3. Hata hivyo, hatua hii inawanufaisha watu wenye ulemavu walio katika umri wa kuajirika.

Vilevile, Serikali imeendelea kutoa mikopo isiyo na riba kwa vikundi vya watu wenye ulemavu kupitia mikopo ya asilimia 10 ya Halmashauri ambapo asilimia 2 hutengwa kwa ajili yao. Hadi kufikia Januari, 2023, jumla ya vikundi vya watu wenye ulemavu 4,761 wakiwemo wanawake wazee wenye ulemavu walipatiwa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 19.58 kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo kilimo, ufugaji, uvuvi, biashara, ushonaji na ususi. Hii ni fursa kwa watu wenye ulemavu kupata mikopo japokuwa kundi hili la wazee wenye ulemavu kwa uhalisia wake sio kundi la uzalishaji, isipokuwa linaweza kupewa ruzuku kwa ajili ya shughuli ndogo ndogo za kujikimu kimaisha.

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa tamko hilo, bado kuna changamoto mbalimbali zikiwemo: Kutokujumuishwa kwa kundi la wanaume wazee wenye ulemavu kwenye suala hilo, hivyo kukosa msukumo wa kisera na matamko yanayoshughulikia kundi hilo; Kuendelea kuwepo kwa mila na desturi zinazowanyanyapaa wazee wenye ulemavu; Sera imeainisha umuhimu wa kujumuishwa kwa wanawake wazee wenye ulemavu katika miradi ya uzalishaji hata hivyo katika Taarifa ya Tathmini imebainisha kuwa kundi hili halikupaswa kupewa jukumu la uzalishaji isipokuwa kuwapa fursa ya kujishughulisha, kujipatia kipato cha kujikimu, kutumia ujuzi walio nao ili kuwafanya wasiwe na maisha bwete.

#### 1.2.1.10 Uzalishaji Mali

Wazee ni kundi muhimu katika jamii kutokana na ujuzi na uzoefu walio nao katika shughuli za uzalishaji mali. Sera ya Taifa ya Wazee ya mwaka 2003 ilibainisha kuwa wazee ni miongoni mwa watu maskini zaidi katika jamii hata hivyo sera hiyo ikaweka mikakati ya kuhamasisha mzee mmoja mmoja au vikundi kuanzisha miradi ya uzalishaji mali mahali walipo na Halmashauri za Wilaya na Wakala za Hiari kujumuisha vikundi vilivyoanzishwa na wazee katika programu zilizopo za uzalishaji mali katika jamii.

Taarifa ya Tathmini ya utekelezaji wa Sera imebainisha kuwepo kwa ujuzi na uzoefu unaotokana na kazi walizokuwa wakizifanya kabla ya umri wa uzee wao. Aidha, ujuzi na uzoefu huo unahitaji kuendelezwa na kutumika. Katika utekelezaji wa sera hiyo Serikali kupitia mashirika ya wazee imeendelea kuhamasisha wazee kujiunga katika vikundi na kufanya shughuli za uzalishaji ili kujikimu kimaisha. Kupitia vikundi hivyo, wazee wameunganishwa na taasisi za mikopo kama vile Benki ya TCB ili kujiendeleza na kuinua kipato ambapo hadi kufikia Juni, 2023 jumla wazee 92,204 wamenufaika na mikopo kutoka taasisi za fedha kupitia mifuko ya hifadhi ya jamii ya PSSSF na NSSF.

Vilevile, Serikali kwa kushirikiana na wadau imewezesha uanzishwaji wa vikundi vya uzalishaji mali kwa wazee ili kuwasaidia kujikwamua kutoka hali duni ya maisha. Serikali imeanzisha vikundi 395 vya uzalishaji mali vya wazee katika mikoa ya Ruvuma, Kigoma, Mwanza, Geita, Mbeya, Tanga, Kagera na Njombe, ambapo jumla ya wazee 10,926 (Me 5,333 na Ke 5,593) walinufaika na miradi ya kukopeshwa mifugo, kilimo na uvuvi.

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, bado kuna changamoto mbalimbali ikiwemo:

(i) Wazee walio wengi kukosa fursa za mikopo kutoka taasisi za fedha kutokana na dhana kuwa wazee hawakopesheki;

(ii) Kukosekana kwa maandalizi ya kuelekea uzeeni yanayosababisha matumizi yasiyo na manufaa kwa baadaye;

(iii) Kukosekana kwa elimu ya ujasiriamali kwa wazee katika kutumia ujuzi na uzoefu wao katika kuwekeza kwenye miradi ya kujikimu na kuwaongezea kipato inayoendana na elimu na ujuzi wao; na

(iv) Kukosekana kwa mfumo rasmi wa kuwatambua wazee wenye uzoefu na ujuzi ili kuweza kutumia ujuzi na uzoefu wao katika nyanja mbalimbali za uchumi na uzalishaji.

#### 1.2.1.11 Mahitaji ya Msingi ya Maisha ya Uzeeni

Uzee na kuzeeka kunaambatana na upungufu wa uwezo wa mwili kufanya kazi, hivyo kusababisha maisha duni kwa badhi ya wazee kutokana na kukosa mahitaji ya msingi. Sera ya Taifa ya Wazee ya mwaka 2003 imeelekeza Serikali kwa kushirikiana na wadau kuwatambua wazee wenye mahitaji ya msingi, kuweka taratibu za utoaji wa huduma na kuzihamasisha familia na jamii zishiriki katika mipango ya uzalishaji mali ili kuinua uwezo wa kuwahudumia wazee. Katika utekelezaji wa matamko hayo, mafanikio kadhaa yamepatikana yakijumuisha Serikali kuendelea kuwatambua wazee wasio na uwezo na kuwapatia huduma mbalimbali. Hadi mwezi Januari, 2023, jumla ya wazee 2,203,414 (Me 1,005,076 na Ke 1,198,338) walikuwa wametambuliwa. Kati ya hao, wazee wasio na uwezo 1,256,544 wamepatiwa vitambulisho vya matibabu bila malipo.

#### 1.2.1.12 Ushirikishwaji wa Wadau

Serikali inatambua na kuthamini mchango wa wadau katika kuhudumia wazee na hivyo kuendelea kutoa ushirikiano kwa lengo la kuboresha maisha ya wazee nchini. Katika kutekeleza lengo hili, vyama vya wazee 42 vimesajiliwa na hivyo hushirikiana na Serikali katika kutoa huduma za msingi kwa wazee. Vilevile, Serikali imeweka mazingira wezeshi kwa wadau kuanzisha na kuendesha makazi binafsi 15 ya wazee na wasiojiweza, kuratibu na kuazimisha Siku ya Wazee Duniani pamoja na Siku ya Kimataifa ya Kupinga Ukatili Dhidi ya Wazee ambapo elimu kwa jamii kuhusu haki na ustawi wa wazee nchini hutolewa. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na wadau imeandaa miongozo na mikakati muhimu ya utoaji wa huduma na ulinzi kwa wazee.

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, jitihada hizi zimekabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo: -

(i) Kukosekana kwa uwiano katika mtawanyiko wa vyama na mashirika ya wazee nchini ambapo sehemu kubwa ya mashirika yamejikita katika maeneo ya mijini; na

(ii) Masuala ya wazee kutopewa kipaumbele na wadau wa maendeleo.

### 1.2.2 Muhtasari wa Yaliyojitokeza kwenye Hali Ilivyo ya Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mwaka 2003

#### 1.2.2.1 Mafanikio

Taarifa ya Tathmini ya Utekelezaji wa Sera ya Mwaka 2003 ilionesha mafanikio katika kukuza ustawi wa wazee nchini. Mafanikio hayo ni pamoja na:

(i) Kuimarika kwa huduma za matunzo na kuongezeka kwa umri wa kuishi ambapo kwa mujibu wa Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa ya Mwaka 2022 katika mwaka 2021 inaonesha kuwa umri wa Mtanzania

wa kuishi umeongezeka na kufikia miaka 66.2 ikilinganishwa na umri miaka 52.6 mwaka 2003 hali iliyochangiwa na; kuimarika kwa huduma za matunzo kwa wazee; kupungua kwa mauaji ya wazee kutoka 203 mwaka 2017 hadi kufikia 130 mwaka 2022; na kuanzishwa kwa madirisha mahsusi ya kuhudumia wazee katika vituo vya afya ambapo hadi kufikia mwaka 2022/2023 jumla ya madirisha 629 yameanzishwa; na

(ii) Kuimarika kwa ustawi wa wazee kulikochangiwa na ushiriki wa wazee katika vikundi vya kujiongezea kipato, ambapo hadi kufikia mwaka 2023 jumla ya vikundi 395 vyenye jumla ya wazee 10,926 (Me 5,333 na Ke 5,593) vilinufaika na miradi ya kukopeshwa mifugo, kilimo na uvuvi.

#### 1.2.2.2 Upungufu

Taarifa ya Tathmini ya Sera ya Taifa ya Wazee ya Mwaka 2003 ilibainisha upungufu uliosababisha kutokufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa kwenye sera hiyo. Upungufu huo ni pamoja na:

(i) Kukosekana kwa eneo na matamko mahsusi ya kushughulikia eneo la miundombinu rafiki na mazingira wezeshi kwa wazee ili kufikia huduma stahiki na kwa wakati;

(ii) Kukosekana kwa eneo linatoa maelezo juu ya huduma za afya ya akili na msaada wa kisaikolojia;

(iii) Kukosekana kwa eneo mahsusi kuhusu uwakilishi wa wazee katika vyombo vya maamuzi;

(iv) Kutojumuishwa kwa eneo la teknolojia ambalo litarahisisha shughuli mbalimbali za wazee;

(v) Kutojumuishwa kwa wanaume wazee kama kundi linaloathiriwa na mila, Imani na desturi potofu;

(vi) Sera kutojumuisha kundi la wanaume wazee wenye ulemavu;

(vii) Sera kutojumuisha makundi rika yote katika kujiandaa na maisha ya uzeeni;

(viii) Sera kutojumuisha masuala mtambuka; na

(ix) Kutojumuishwa kwa mipango mipya ya maendeleo ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa iliyoandaliwa baada ya Sera hii kutungwa. Mipango hiyo ni pamoja na: Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025); Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu (2011/12 – 2025/26); Malengo ya Maendeleo Endelevu (2030); na Agenda ya Afrika Tuitakayo (2063).

#### 1.2.2.3 Changamoto

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Sera hiyo, upo upungufu na changamoto zilizojitokeza ambao umetokana na kutokuwepo kwa masuala mahsusi ya kisera katika Sera hiyo kama ifuatavyo:

(i) Kukosekana kwa huduma jumuishi za kiafya na wataalam wa afya bobezi wenye ubingwa (*geriatrician*) mahsusi kwa wazee;

(ii) Kuendelea kuwepo kwa maradhi yanayotokana na mtindo wa maisha ikiwemo maisha bwete na ulaji unaosababisha madhara uzeeni;

(iii) Matunzo duni kwa wazee katika ngazi ya familia na jamii yanayosabishwa na umaskini na vitendo vya utelekezaji kwa wazee;

(iv) Kuendelea kuwepo kwa vitendo vya ukatili vinavyosababishwa na mila na imani potofu zinazoendeleza kuwepo kwa utelekezaji, ubaguzi, unyanyasaji na mauaji dhidi ya wazee;

(v) Uchangiaji mdogo katika mifuko ya hifadhi ya jamii unaosababishwa na uelewa mdogo wa jamii kuhusu umuhimu wa kuweka akiba ya uzeeni;

(vi) Ushiriki mdogo wa wazee katika kutumia ujuzi na uzoefu wao katika shughuli za ujasiriamali jamii;

(vii) Wazee kutokuendana na mabadiliko na kukua kwa teknolojia;

(viii) Uelewa mdogo wa jamii juu ya namna ya kukabiliana na changamoto mbalimbali za afya ya akili kwa wazee na jamii inayowahudumia;

(ix) Kukosekana kwa uwakilishi wa kundi la wazee kwenye vyombo mbalimbali vya uamuzi hivyo kutokujumuishwa kwa ajenda zao kwenye mipango ya maendeleo;

(x) Kutozingatiwa kwa ujenzi wa miundombinu wezeshi kwa wazee kwenye majengo na makazi binafsi; na

(xi) Kuendelea kuwepo kwa mila na desturi potofu zinazokandamiza upande mmoja wa jinsia.

Kutokana na upungufu na changamoto zilizobainishwa katika utekelezaji wa Sera ya Mwaka 2003, upo umuhimu wa kufanya marekebisho ya Sera hii ili kuzingatia na kujumuisha afua na maudhui yaliyomo katika Mipango, Dira, Mikataba, Maazimio, Itifaki, sera na sheria mbalimbali katika ngazi ya Kimataifa, Kikanda na Kitaifa ambazo zimeridhiwa, zimetungwa na zinazotekelezwa na nchi ili kutatua changamoto zilizobaishwa.

### 1.2.3 Maeneo Ambayo Hayakujumuishwa Kwenye Sera ya Wazee (2003)

Taarifa ya tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Wazee imebaini maeneo ya kisera ambayo hayakujumuishwa wakati wa kuandaliwa kwa Sera ya mwaka 2003. Maeneo hayo ni kama ifuatavyo:

#### 1.2.3.1 Miundombinu na Mazingira Wezeshi kwa Wazee

Miundombinu na mazingira wezeshi ni suala la msingi kwa wazee ili waweze kufikia huduma mbalimbali kwa urahisi zikiwemo za matibabu,

huduma za fedha, usafiri, maji safi na salama na vyoo katika maeneo ya umma na binafsi. Hali ya uzee inaambatana na changamoto za kiafya zinazosababisha kushindwa kuyamudu mazingira. Hivyo, upo umuhimu wa kuwa na miundombinu rafiki kwa wazee katika maeneo yote ya huduma kama vile maeneo ya michezo na mapumziko kwa wazee.

Serikali imeweka miongozo ya kuzingatia kwa makundi maalumu wakiwemo wazee katika maeneo ya kutolea huduma ikiwa ni pamoja na kuzingatia ujenzi wa miundombinu rafiki itakayorahisisha ufikiaji wa huduma kwa wazee. Vilevile, imeanzisha na kuendesha kampeni mbalimbali za kuhakikisha mzee anapewa kipaumbele katika kupata huduma. Moja ya kampeni hizo ni “Mpishe Mzee kwanza” ambayo imeleta tija kwa wazee kufikia huduma za afya kwa urahisi. Aidha, jumla ya madirisha 629 yameanzishwa kwa ajili ya kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa wazee katika vituo vya kutolewa huduma za afya.

Sera ya Afya (2007) na Sera ya Watu Wenye Ulemavu (2003) zimetambua kundi la watu wenye ulemavu kuwa ni kundi lenye changamoto katika ufikiaji wa huduma kutokana na miundombinu isiyo rafiki. Hata hivyo, kundi la wazee halikutajwa katika sera hizi, licha ya wazee kuwa kundi lenye changamoto katika kuzifikia huduma kutokana na miundombinu isiyo rafiki. Hali hii inasababisha wazee kushindwa kunufaika na huduma za kijamii. Pamoja na kwamba Serikali inaelekeza ujenzi uzingatie mahitaji maalum, bado kuna baadhi ya miundombinu ya umma haizingatii ujenzi na mazingira yanayorahisisha ufikiaji wa huduma kwa wazee. Asilimia 99 ya waliohojiwa katika taarifa ya tathmini ya mahitaji ya wazee walipendekeza suala la miundombinu rafiki na mazingira wezeshi kuzingatiwa katika Sera ya Wazee. Masuala hayo ni pamoja na kuwepo kwa madirisha maalum ya

kuhudumia wazee katika huduma mbalimbali za kijamii na wazee kupewa kipaumbele katika vyombo vya usafiri.

Hivyo, upo umuhimu wa Sera hii kupanua wigo na kuweka matamko ya kuhakikisha kuwa kundi la wazee linajumuishwa katika ufikiaji wa miundombinu rafiki katika majengo ya umma na binafsi.

#### 1.2.3.2 Wazee na Teknolojia

Kati ya mwaka 2005 na 2013, kumekuwa na ongezeko la kasi katika umiliki na upatikanaji wa Teknolojia za Habari na Mawasiliano (TEHAMA) duniani. Umiliki wa TEHAMA nchini Tanzania pia umeonesha ukuaji kati ya mwaka 2001 na 2007 hasa katika matumizi ya simu za mikononi ambayo yalikua kutoka asilimia 1 mwaka 2001 hadi asilimia 25 mwaka 2007, ikiwa ni ukuaji wa zaidi ya asilimia 2000. Ilipofika mwaka 2012 kiwango cha umiliki wa simu za mkononi Tanzania kilifikia asilimia 61. Hata hivyo, kwa mujibu wa takwimu za Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (Tanzania Communication Regulating Authority – TCRA), kasi ya kupenyeza kwa mtandao wa intaneti ilikuwa ni ndogo zaidi ikitokea asilimia 4.5 mwaka 2005 hadi asilimia 16.8 mwaka 2012. Matarajio makubwa kwa jamii yetu ni kuwa na wazee wanaoishi katika mazingira ambayo ni rafiki na yenye upatikanaji wa huduma stahiki kulingana na mabadiliko ya kila siku katika nyanja zote. Aidha, kutokana na kukua kwa sayansi na teknolojia, Serikali na jamii imekuwa ikutumia mifumo mbalimbali ya kidijitali katika shughuli za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni. Kwa kuwa matumizi ya sayansi na teknolojia kwa sasa nchini hayaepukiki, ipo haja ya kundi la wazee kupewa kipaumbele katika matumizi ya sayansi na teknolojia kwani kwa kuwa kundi hili lipo nyuma katika kupokea mabadiliko hayo.

Asilimia 97.9 ya waliohojiwa katika Tathmini ya Mahitaji ya Wazee walipendekeza suala la teknolojia kwa wazee kuzingatiwa katika Sera ya Taifa ya Wazee ya Mwaka 2003, Toleo la Mwaka 2024. Aidha, asilimia 83.5 walipendekeza kuwe na utaratibu wa wazee kupatiwa mafunzo kuhusu teknolojia mbalimbali zinazojitokeza. Vilevile, asilimia 1.9 walipendekeza wazee kuwezeshwa kutumia teknolojia katika shughuli zao za kila siku.

#### 1.2.3.3 Huduma za Afya ya Akili na Msaada wa Kisaikolojia na Kijamii

Afya ya akili ni hali ya kuwa sawa kiakili na kisaikolojia au kutokuwa na msongo wa mawazo. Wazee wengi wanakabiliwa na changamoto ya afya ya akili kutokana na changamoto mbalimbali zinazoambatana na hali ya uzee ikiwemo hofu na wasiwasi, msongo wa mawazo, sonona, upweke, huzuni, unyanyapaa na magonjwa ya kuambukiza na yasiyoambukiza. Msaada wa kisaikolojia ni mojawapo ya huduma za msingi katika kuimarisha afya na ustawi wa wazee.

Taarifa ya tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Wazee ya Mwaka 2003 ilibaini kuwa uwezo wa wazee kustahimili changamoto za maisha ni mdogo, hivyo kupoteza matumaini na mwelekeo katika maisha. Kuwajengea wazee ustahimilivu, kupitia huduma za afya ya akili na msaada wa kisaikolojia kutaongeza uwezo wao wa kuendelea kuishi bila kukata tamaa. Matatizo mengi ya kiafya na kimahusiano yanayowakabili wazee yanatibika kikamilifu kupitia msaada wa kisaikolojia na kijamii. Pamoja na juhudi za Serikali katika kutoa huduma hii, bado kuna umuhimu wa kuimarisha mfumo wa utoaji wa huduma hii nchini ili wananchi wote wakiwemo wazee waweze kuzifikia kwa urahisi.

Vilevile, katika Tathmini ya Mahitaji ya Wazee, asilimia 98.1 ya wahojiwa walipendekeza kuimarishwa kwa huduma ya msaada wa kisaikolojia na kijamii kwa wazee ili kuondokana na changamoto za msongo wa mawazo, upweke na hivyo kuwajengea ustahimilivu. Aidha, asilimia 9.8 ya waliohojiwa walipendekeza kuanzishwa kwa klabu za michezo na burudani kwa wazee kama njia ya kupunguza changamoto hizo. Vilevile, asilimia 10 ya waliohojiwa walipendekeza kutolewa kwa elimu kwa jamii kuhusu masuala ya upweke na msongo wa mawazo kwa wazee ili jamii iwe na ujuzi wa kuweka mazingira yatakayozuia wazee kupata changamoto hizo na jinsi ya kukabiliana nazo.

#### 1.2.3.4 Masuala Mtambuka ya Sera

Tathmini ya Sera iliyofanyika ili kubaini kuwa jinsia na VVU na UKIMWI ni masuala mtambuka katika ustawi wa wazee yaani yanatekelezwa kwa kushirikiana na sekta na mamlaka nyingine kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizopo.

Suala la uzingatiaji wa jinsia ni muhimu katika kuleta haki na wajibu wa wanawake na wanaume wazee. Wanawake wazee wanapitia changamoto ngumu zaidi kwa sababu ya jinsi yao, kwa mfano baadhi ya mila na desturi zetu zimewabebesha wanawake wazee mzigo mkubwa wa malezi katika familia. Aidha, mfumo dume katika jamii nyingi umekuwa unamnyima mwanamke mzee haki ya kumiliki mali sawa na mwanaume mzee. Kwa upande mwingine mila potofu zimeendeleza vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake ikiwemo mauaji ya wanawake wazee. Hivyo, ni muhimu kujumuisha masuala ya jinsia katika uandaaji, upangaji, utoaji uamuzi na utekelezaji wa Sera ya Wazee.

Uharibifu wa mazingira kwa kiasi kikubwa huchangiwa na kuwepo kwa shughuli mbalimbali za kibinadamu mathalani uvunaji wa mazao ya asili, shughuli za viwanda, kilimo, madini, uvuvi na ufugaji. Shughuli hizi zinapotekelezwa bila kuzingatia athari za mazingira husababisha uharibifu mkubwa wa mazingira. Uhusiano huu wa mazingira na shughuli za kiuchumi huathiriwa na changamoto mbalimbali ikiwemo mabadiliko ya tabianchi, matumizi mabaya ya rasilimali za asili, uvunaji wa mazao ya asili usiozingatia uhifadhi wa mazingira, matumizi ya mbinu duni za kilimo, uvamizi na uharibifu wa vyanzo vya maji, kupungua kwa rasilimali za asili kama vile maji na mazao ya misitu yakiwemo kuni na mkaa kwa matumizi ya nyumbani na hivyo kusababisha changamoto ya afya kwa wazee. Changamoto hizo ni pamoja na matatizo kwenye mifumo ya ya upumuaji na macho makundu ambayo kwa baadhi ya maeneo yamehusishwa na imani za kishirikina na kusababisha vifo kwa baadhi ya wazee.

Suala la VVU na UKIMWI pia limeonekana kuathiri zaidi makundi tete ikiwemo wazee. Kwa mfano, wazee kubeba jukumu la kulea watoto yatima walioachwa na wazazi wao kutokana na ugonjwa wa UKIMWI. Aidha, Sera ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI (2001), inaelekeza kuwa wazee wanapaswa kupatiwa huduma za matibabu wao wenyewe na kuwatunza wajukuu walioachiwa.

# SURA YA PILI

# UMUHIMU WA SERA, DIRA, DHIMA NA MALENGO

## 2.1 Umuhimu wa Sera

Sera ya Taifa ya Wazee ya mwaka 2003 ililenga katika kuhakikisha kuwa wazee wa Tanzania wanatambuliwa na kupewa fursa ya kushiriki katika mambo yanayohusu maisha yao ya kila siku kwa manufaa yao na ya Taifa kwa ujumla na wanapata huduma zote muhimu na za msingi zitakazowawezesha kushiriki kikamilifu katika maisha yao ya kila siku. Sera ilianisha kushughulikia maeneo 15 ambayo ni: Huduma za afya, matunzo ya wazee, wanawake wazee na mila zilizopitwa na wakati, hifadhi ya jamii, mabaraza ya wazee, malezi na maandalizi ya vijana kuelekea uzeeni, mahitaji ya msingi ya maisha ya uzeeni, elimu, vyama vya kuhudumia wazee, wanawake wazee wenye ulemavu, sheria zisizolinda na kuendeleza maslahi ya wazee, ushirikishwaji wa wazee, ushirikishwaji wa wadau na mfuko wa wazee.

Hata hivyo, katika utekelezaji wa sera hiyo tathmini ilibainisha kuwepo kwa mafanikio, changamoto, upungufu na masuala ambayo hayakujumuishwa na yanayohitaji kurekebishwa ili kuimarisha upatikanaji wa huduma za matunzo, ustawi na ulinzi kwa wazee katika jamii. Kwa msingi huu, Sera ya Taifa ya Wazee ya mwaka 2003 Toleo la Mwaka 2024 itawawezesha wazee kuishi maisha bora yenye tija na kushiriki kikamilifu katika ustawi wa maendeleo yao binafsi na maendeleo ya nchi kwa ujumla.

## 2.2 Dira, Dhima na Malengo ya Sera

### 2.2.1 Dira

Kuwa na Taifa ambalo wazee watakuwa na fursa ya kuishi maisha toshelevu.

### 2.2.2 Dhima

Kuhakikisha kuwa huduma za matunzo, ustawi na ulinzi kwa wazee zinatolewa kwa ufanisi na kuzingatia uwiano, haki, usawa na viwango vya ubora endelevu.

### 2.2.3 Malengo ya Sera

#### 2.2.3.1 Lengo Kuu

Kuimarisha upatikanaji wa huduma za matunzo, ustawi na ulinzi kwa wazee katika familia, jamii na taasisi mbalimbali.

#### 2.2.3.2 Malengo Mahsusi

(i) Kuhakikisha upatikanaji wa huduma jumuishi za afya kwa wazee;

(ii) Kuboresha matunzo ya wazee katika ngazi ya familia na jamii;

(iii) Kuimarisha ulinzi na usalama wa wazee;

(iv) Kuimarisha maandalizi ya jamii kwa ajili ya maisha ya uzeeni;

(v) Kuongeza ushiriki wa wazee katika kutumia uzoefu na ujuzi walionao ili kuongeza kipato cha kujikimu na kuimarisha afya na ustawi wao;

(vi) Kuimarisha matumizi ya teknolojia kwa ustawi wa wazee;

(vii) Kuimarisha afya ya akili na utoaji wa msaada wa kisaikolojia kwa wazee ili kustahimili changamoto za uzeeni;

(viii) Kuimarisha ushiriki wa wazee katika mipango ya maendeleo na masuala kijamii kwenye ngazi mbalimbali za Serikali;

(ix) Kuweka miundombinu na mazingira wezeshi kwa wazee kufikia huduma;

(x) Kuhakikisha mipango na programu mbalimbali kuhusu huduma kwa wazee zinazingatia jinsia;

(xi) Kukuza ushiriki wa wazee katika masuala ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira; na

(xii) Kuhakikisha wazee wanafikiwa na huduma mahsusi za Virusi vya Ukimwi (VVU) na Upungufu wa Kinga Mwilini (UKIMWI).

# SURA YA TATU

# HOJA NA MATAMKO YA SERA

## 3.1 Utangulizi

Serikali kwa kushirikiana na wadau ina jukumu la kuhakikisha wananchi wanakuwa na uelewa kuwa ni jukumu lao kuendelea kushiriki kikamilifu katika shughuli za uzalishaji mali na kuboresha ustawi wa maisha yao hata katika kipindi cha kuingia uzeeni. Katika Sera hii, suala kubwa la msingi ambalo limezingatiwa ni kutengeneza mikakati ya kuhakikisha kuwa wazee wanawezeshwa kuendelea kutumia ujuzi, weledi na uzoefu wao katika ubunifu wa miradi, shughuli za uzalishaji mali na burudani.

Serikali imeendelea kuwatambua na kuwapa fursa wazee kushiriki katika shughuli za uzalishaji mali ili kuchangia kikamilifu katika ustawi na maendeleo yao wenyewe na kwa manufaa ya watanzania wote. Katika kufikia azma hii, Serikali ina jukumu la kuandaa sera, miongozo na mapendekezo ya sheria kadri itakavyoonekana inafaa yatakayosimamia utoaji na upatikanaji wa haki na huduma muhimu kwa wazee. Sera hii inaweka msingi na mwelekeo wa kuwandaa wananchi kuingia na kuishi maisha ya furaha na kuheshimika katika kipindi cha uzeeni kwa kuendelea kushiriki kikamilifu katika nyanja mbalimbali kulingana na vipaji na uwezo wao.

Aidha, Sera hii inalenga kuondoa mtazamo hasi katika jamii kuwa maisha ya uzeeni ni kiashiria cha kupungukiwa uwezo wa kushiriki shughuli za uzalishaji mali na kijamii. Mwelekeo wa Sera hii unatambua umuhimu wa wazee kuendelea kuishi maisha bora na yenye tija kupitia miradi ya ubunifu ya uzalishaji mali, burudani, mazoezi, vikundi vya msaada wa kisaikilojia na kijamii. Sera hii pia inatoa maelezo na matamko kuhusu afua mbalimbali za

kuwezesha wazee kuendelea kushiriki kikamilifu katika ustawi na maendeleo yao binafsi na ya nchi kwa ujumla kama ifuatavyo:

## 3.2 Masuala ya Kisera

### 3.2.1 Huduma za Afya kwa Wazee

Uhakika wa upatikanaji wa huduma jumuishi za afya kwa wazee ni haki yao ya msingi. Pamoja na mafanikio ya kuwepo kwa Sera ya Afya inayotambua kundi hilo kwa kuwapatia msamaha wa matibabu na uwepo wa madirisha mahsusi ya wazee, bado kuna upungufu wa wataalam wabobezi na wenye ubingwa mahsusi kwa wazee (*geriatrician)* ikilinganishwa na makundi mengine yenye wataalam mahsusi wa makundi hayo kama vile watoto na wanawake. Vilevile, mtindo wa maisha unachangia kiasi kikubwa athari za kiafya wakati wa uzee ambao husababisha magonjwa yasiyoambukiza kama kisukari na shinikizo la damu. Hata hivyo, masuala ya kuwawezesha wazee kujikinga na changamoto zinazosababisha maradhi yanapaswa kupewa kipaumbele. Hivyo, Sera hii pamoja na mambo mengine inalenga katika kutekeleza afua za kiustawi za kuzuia maradhi yanayoambatana na uzee.

**Lengo**

Kuhakikisha upatikanaji wa huduma jumuishi za afya kwa wazee.

**Matamko ya Sera**

| |
|---|
| Serikali kwa kushirikiana na wadau itafanya yafuatayo:<br>(i) Kuimarisha huduma za kinga na tiba dhidi ya magonjwa yanayoambatana na uzee;<br>(ii) Kukuza uelewa kwa wazee kuhusu masuala ya afya na lishe; na<br>(iii) Kuimarisha mifumo ya kukabiliana na magonjwa ya mlipuko, magonjwa yasiyo ambukiza na yanayoambukiza. |

### 3.2.2 Matunzo Kwa Wazee

Uhakika wa upatikanaji wa matunzo kwa wazee ni suala la msingi ili waendelee kuishi maisha bora. Azimio la Umoja wa Mataifa Na. 46 la Mwaka 1991 linawatambua wazee kuwa na haki ya kupatiwa matunzo na familia, ndugu na jamii. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Sera hiyo, Taarifa ya Tathmini ilibaini kuwa mabadiliko ya kijamii na kiuchumi yamesababisha kudhoofika kwa mifumo ya asili ya matunzo kwa wazee, na hivyo wazee hususan wanaoishi vijijini wamekuwa wakiishi katika hali duni. Hali hii imechochewa na kukua kwa miji ambayo imesababisha vijana kukimbilia mijini na kuwaacha wazee bila msaada katika familia na jamii. Pamoja na kuwa jamii imeendelea kuhamasishwa kutekeleza wajibu wao katika kuwahudumia wazee, zipo changamoto ya utelekezaji wa wazee katika familia na jamii.

**Lengo**

Kuboresha matunzo ya wazee katika ngazi ya familia na jamii.

**Matamko ya Sera**

Serikali kwa kushirikiana na wadau itafanya yafuatayo:

(i) Kuweka na kusimamia mifumo ya kuhakikisha familia na jamii inawajibika ipasavyo kuwatunza wazee wao;

(ii) Kuimarisha mifumo na kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika kuwahudumia wazee wasiojiweza na wasio na ndugu wa kuwahudumia; na

(iii) Kukuza uelewa wa familia na jamii kuhusu huduma na ustawi kwa wazee.

### 3.2.3 Ulinzi na Usalama wa Wazee

Ulinzi na usalama wa wazee wa jinsi zote ni jukumu la kila mtu katika familia na jamii. Ulinzi na usalama ni pamoja na kuzuia vitendo vya ukatili na unyanyasaji kwa wazee hususan mauaji ya wazee kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo imani za kishirikina ambazo zimeendelea kuwa changamoto katika familia na jamii. Kutokana na Taarifa ya Tathmini ya matukio ya ukatili yameendelea kutokea ikiwemo mauaji ya wazee ambapo kwa mwaka 2020 kulikuwa na jumla ya matukio 54, kwa mwaka 2021 hakukuwa na matukio yoyote ya mauaji ya wazee, kwa mwaka 2022 matukio ya mauaji kwa wazee yameongezeka hadi kufikia 130. Kutokana na hali hii, upo umuhimu wa kuendelea kuongeza juhudi za kukabiliana na changamoto za utelekezaji, ubaguzi, unyanyasaji na mauaji dhidi ya wazee.

**Lengo**

Kuimarisha ulinzi na usalama wa wazee.

**Matamko ya Sera**

| |
|---|
| Serikali kwa kushirikiana na wadau itafanya yafuatayo:<br>(i) Kuboresha ulinzi shirikishi katika familia na jamii ili kuwalinda wazee dhidi ya vitendo vya ukatili;<br>(ii) Kuhakikisha wazee manusura wa ukatili wanapata huduma za msingi;<br>(iii) Kuimarisha uelewa wa familia na jamii kuhusu imani, mila na desturi hasi zinazolenga ubaguzi, unyanyasaji na mauaji ya wazee; na<br>(iv) Kuimarisha mifumo ya kisheria ya kuwalinda wazee. |

### 3.2.4 Umuhimu wa Jamii Kujiandaa Kabla ya Kufikia Uzee

Umuhimu wa jamii kujiandaa kabla ya kuzeeka ni suala la kuzingatiwa wakati wote katika shughuli za kuzalisha mali na maisha ya kila siku. Pamoja na jitihada mbalimbali za uwezeshaji wa vijana bado kuna changamoto ya uelewa mdogo wa maandalizi kuelekea uzeeni kutokana na vijana kutokuona umuhimu wa kutumia fursa walizonazo za nguvu kazi kuwekeza kwa ajili ya maisha ya uzeeni. Vilevile, kukosekana kwa utaratibu maalumu wa kuelimisha jamii kujiandaa na maisha ya uzeeni kwa kuzingatia mzunguko wa maisha ya binadamu kuanzia ngazi ya utotoni hadi uzeeni. Aidha, uwekaji wa akiba kwa vijana umeendelea kuwa ni changamoto inayosababishwa na hali duni ya maisha hususan kwa vijana wenye ajira zisizo rasmi. Hivyo, kuna umuhimu wa Serikali kuweka jitihada zaidi za maandalizi ya rika zote kuelekea uzeeni.

**Lengo**

Kuimarisha maandalizi ya jamii kwa ajili ya maisha ya uzeeni.

**Tamko la Sera**

| |
|---|
| Serikali kwa kushirikiana na wadau itafanya yafuatayo:<br>(i) Kukuza uelewa wa jamii na wadau kuhusu umuhimu wa kuweka mipango ya maandalizi ya maisha ya uzeeni; na<br>(ii) Kuhamasisha jamii kujiwekea akiba wakati wa ujana kwa ajili ya maisha ya uzeeni. |

### 3.2.5 Ujasiriamali Jamii kwa Wazee

Ujasiriamali jamii kwa wazee ni dhana inayosisitiza umuhimu wa wazee katika uthubutu wa kutumia ujuzi, fani na uzoefu wao ili kuwekeza katika miradi au shughuli za kujiongezea kipato. Kufikia umri wa miaka 60 haina maana kwamba uwezo wa kufanya kazi umekwisha. Wazee wengi

wanakosa uthubutu wa kuendeleza ujuzi, fani na uzoefu wao waliotoka nao kwenye maeneo ya kazi hususan wazee wastaafu. Pamoja na jitihada zilizofanyika, bado eneo la ujasiriamali jamii limekuwa na changamoto kwa wazee kukosa fursa za mikopo kutoka taasisi za kifedha kutokana na dhana kuwa wazee hawakopesheki; kukosekana kwa elimu ya ujasiriamali na maandalizi kabla ya kuingia uzeeni; na kukosekana kwa mfumo rasmi wa utambuzi wa wazee wenye uzoefu na ujuzi ili kuweza kutumia ujuzi na uzoefu wao.

Wazee kupewa nafasi ya kutumia ujuzi na uzoefu na kuendelea kuwezeshwa kufanya shughuli ni dhahiri kuwa watafanikiwa kuendelea kupata kipato cha kujikimu. Vilevile, ni muhimu kulizingatia eneo hili ili wazee waweze kukidhi mahitaji yao pia itakuwa ni sehemu ya mazoezi kwa ajili ya kujiimarisha afya.

**Lengo**

Kuongeza ushiriki wa wazee katika kutumia uzoefu na ujuzi walionao ili kuongeza kipato cha kujikimu na kuimarisha afya na ustawi wao.

**Matamko ya Sera**

Serikali kwa kushirikiana na wadau itafanya yafuatayo:

(i) Kuanzisha na kusimamia mfumo wa utambuzi wa wazee wenye ujuzi, taaluma na maarifa asilia ili kufaidika na uzoefu wao;

(ii) Kuweka na kusimamia utaratibu wa kuwezesha wazee kutumia ujuzi na uzoefu wao katika ujasiriamali jamii ili kujikimu;

(iii) Kuweka na kusimamia utaratibu wa kutoa elimu ya ujasiriamali katika rika zote na kujiandaa kuelekea uzeeni; na

(iv) Kuweka na kusimamia mifumo ya kuwawezesha wazee kiuchumi.

### 3.2.6 Wazee na Teknolojia

Matarajio makubwa kwa jamii yetu ni kuwa na wazee wanaoishi katika mazingira rafiki na yenye upatikanaji wa huduma stahiki kulingana na mabadiliko ya kila siku katika nyanja zote. Aidha, kutokana na kukua kwa sayansi na teknolojia, Serikali na jamii imekuwa ikitumia mifumo mbalimbali ya kidijitali katika shughuli za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni (mfano: ulipaji wa ankara za umeme na maji, kutuma na kupokea fedha kwa kutumia simu na kupata elimu ya masuala mbalimbali ya kijamii ikiwemo afya). Kwa kuwa matumizi ya sayansi na teknolojia kwa sasa nchini hayaepukiki, ni muhimu kwa kundi la wazee kupewa kipaumbele katika matumizi ya sayansi na teknolojia kwani kundi hili lipo nyuma katika kupokea mabadiliko hayo. Aidha, maendeleo ya sayansi na teknolojia yamewezesha kuwepo kwa teknolojia mbalimbali zinazoweza kutumika kuwasaidia wazee katika changamoto mbalimbali ikiwemo vifaa vya kusaidia kujongea, kuongeza usikivu na kuona.

**Lengo**

Kuimarisha matumizi ya teknolojia kwa ustawi wa wazee.

**Matamko ya Sera**

Serikali kwa kushirikiana na wadau itafanya yafuatayo:

(i) Kuimarisha upatikanaji na matumizi ya teknolojia rafiki kwa wazee zitakazowasaidia kukabiliana na changamoto zao; na

(ii) Kukuza uelewa kwa wazee ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia na matumizi ya TEHAMA.

### 3.2.7 Huduma za Afya ya Akili na Msaada wa Kisaikolojia na Kijamii

Afya ya akili ni hali ya kuwa sawa kiakili na kisaikolojia au kutokuwepo kabisa kwa msongo wa akili ya mtu, mfano kutokuwa na msongo wa

mawazo. Wazee wengi wanakabiliwa na changamoto ya afya ya akili kutokana na changamoto mbalimbali zinazoambatana na hali ya uzee ikiwemo hofu na wasiwasi, msongo wa mawazo, sonona, upweke, huzuni, unyanyapaa na magonjwa ya kuambukiza na yasiyo ambukiza. Msaada wa kisaikolojia ni mojawapo ya huduma za msingi katika kuimarisha afya na ustawi wa wazee.

Aidha, matatizo mengi ya afya ya akili yanayoyakabili makundi katika jamii hususan wazee yanatibika kikamilifu kupitia huduma ya msaada wa kisaikolojia na kijamii. Taarifa ya Tathmini imebainisha kuwa wapo wazee wengi wanaotelekezwa na ndugu na familia zao hali inayowasababishia upweke, huzuni, msongo wa mawazo na kudhoofisha afya zao. Vilevile, upo uelewa mdogo wa jamii juu ya namna ya kuweza kukabiliana na changamoto mbalimbali za afya ya akili hususan katika kuwahudumia wazee.

**Lengo**

Kuimarisha afya ya akili na utoaji wa msaada wa kisaikolojia kwa wazee ili kustahimili changamoto za uzeeni.

**Matamko ya Sera**

Serikali kwa kushirikiana na wadau itafanya yafuatayo:

(i) Kuimarisha utaratibu wa utatuzi wa awali wa changamoto za afya ya akili kwa wazee;

(ii) Kuimarisha uelewa wa utoaji wa huduma za msaada wa kisaikolojia kwa familia na jamii; na

(iii) Kuhamasisha wazee kushiriki kwenye shughuli za burudani na michezo ili kuimarisha afya ya akili na mwili.

### 3.2.8 Ushirikishwaji wa Wazee katika Mipango ya Maendeleo na Masuala na Masuala ya Kijamii

Ushirikishwaji wa wazee katika masuala muhimu hususan ya kijamii na yanayowahusu wao wenyewe ni muhimu katika kuimarisha maendeleo na ustawi wa jamii. Kutokana na elimu, ujuzi na uzoefu walio nao wazee ni muhimu kuwashirikisha katika mipango mbalimbali ya maendeleo ili kurithisha hazina hiyo kwa jamii. Taarifa ya tathmini imebainisha kuwa pamoja na uwepo wa Mabaraza ya Wazee, bado ushiriki wa wao kwenye mipango ya maendeleo ni mdogo ikilinganishwa na makundi mengine kama vile wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Suala hili linachangia kutozingatiwa kwa utatuzi wa changamoto za wazee.

Serikali inatambua kuwepo kwa Mabaraza ya Ushauri ya Wazee na kuyaendeleza kama chombo muhimu cha kuimarisha ushiriki wa wazee katika mipango ya maendeleo ya jamii. Taarifa ya tathmini imebaini kuwa pamoja na kuwepo kwa mabaraza hayo wazee wanahitaji kurithisha uzoefu, maarifa na ujuzi na kutumia vyombo hivyo ili kujadili changamoto. .

**Lengo**

Kuimarisha ushiriki wa wazee katika mipango ya maendeleo na masuala kijamii kwenye ngazi mbalimbali za Serikali.

**Matamko ya Sera**

Serikali kwa kushirikiana na wadau itafanya yafuatayo:

(i) Kuwawezesha hoja za Baraza la Wazee kujadiliwa kwenye majukwaa ya uamuzi katika ngazi zote Serikalini;

(ii) Kuhakikisha wazee wanashiriki katika uandaaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo katika ngazi mbalimbali;

(iii) Kukuza uelewa kwa jamii juu ya umuhimu wa kuwashirikisha wazee

katika masuala mbalimbali ili kuweza kurithi hazina zao;

(iv) Kuimarisha Majukwaa ya Wazee ikiwemo Mabaraza ya Wazee ili kutoa ushauri wa masuala mbalimbali yanayowahusu wazee na jamii; na

(v) Kuweka mfumo wa kuwatumia wazee katika kusuluhisha migogoro ya kijamii.

### 3.2.9 Miundombinu na Mazingira Wezeshi kwa Wazee

Miundombinu na mazingira wezeshi ni suala la msingi kwa wazee ili waweze kufikia huduma mbalimbali kwa urahisi ikiwemo matibabu, huduma za kifedha, usafiri, maji safi na salama na vyoo katika maeneo ya umma na binafsi. Hali ya uzee inaambatana na changamoto za kiafya zinazosababisha kushindwa kuyamudu mazingira. Hivyo, upo umuhimu wa kuwa na miundombinu rafiki kwa wazee katika maeneo yote ya huduma kama vile maeneo ya michezo na mapumziko kwa wazee.

Katika kuhakikisha kuwa wazee wanapata huduma za msingi, Serikali inaelekeza ujenzi uzingatie mahitaji maalumu ya kundi hilo. Hata hivyo, Taarifa ya Tathmini imebaini uwepo wa changamoto ya baadhi ya miundombinu ya umma na binafsi ambayo haina mazingira yanayorahisisha wazee kufikia huduma.

**Lengo**

Kuweka miundombinu na mazingira wezeshi kwa wazee kufikia huduma.

**Tamko la Sera**

Serikali kwa kushirikiana na wadau itafanya yafuatayo:

(i) Kuboresha miundombinu ya umma na binafsi ili kuhakikisha wazee wanafikia huduma mbalimbali za kijamii; na

| | |
|---|---|
| (ii) | Kuanzisha na kuhamasisha uzingatiaji wa utaratibu wa ujenzi wa miundombinu rafiki kwa wazee. |

### 3.2.10 Masuala Mtambuka ya Sera

Masuala haya yatatekelezwa kwa kushirikiana na sekta na mamlaka nyingine zinazogusa maisha ya wazee. Maeneo haya mtambuka ni pamoja na: Jinsia; Mazingira; Virusi Vya Ukimwi (VVU) na Upungufu wa Kinga Mwilini (UKIMWI).

#### 3.2.10.1 Jinsia

Wanawake wazee wamekuwa wakibeba mzigo mkubwa katika shughuli za uzalishaji mali na malezi katika familia na wanaume wazee wamekuwa wakibebeshwa jukumu la kiuchumi hali inayowasababishia kupungua kwa umri wa kuishi. Aidha, imani, mila na desturi potofu katika jamii nyingi zimekuwa zikimnyima mwanamke mzee haki ya kumiliki mali sawa na mwanaume mzee. Kwa upande mwingine imani, mila na desturi potofu zimeendeleza vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na wanaume ikiwemo mauaji ya wanawake na wanaume wazee. Vilevile, Taarifa ya Tathmini imebainisha kuwepo kwa changamoto ya kukosekana kwa uwiano sawa wa matunzo kwa wazazi wazee kutoka watoto wao hali inayosababisha wanaume wazee kukosa matunzo bora pamoja na kwamba ipo Sheria ya Mtoto, Sura ya 13 inayotoa wajibu kwa mzazi kumtunza mtoto. Hata hivyo, hakuna sheria inayompa wajibu mtoto kumtunza mzazi wake. Hivyo, masuala ya jinsia ni muhimu kujumuisha katika uandaaji, upangaji, utoaji wa huduma maamuzi na utekelezaji wa Sera.

**Lengo**

Kuhakikisha mipango na programu mbalimbali kuhusu huduma kwa wazee zinazingatia jinsia.

**Matamko ya Sera**

| |
|---|
| Serikali kwa kushirikiana na wadau itafanya yafuatayo:<br>i) Kuweka mifumo thabiti inayotoa haki na wajibu kwa watoto kuwatunza wazazi wazee wao;<br>ii) Kuimarisha mifumo ya utoaji haki ikiwemo umiliki wa mali kwenye mirathi kwa kuzingatia usawa kwa wanawake na wanaume; na<br>iii) Kuhamasisha familia na jamii kuweka usawa wa matunzo kwa wazee. |

**3.2.10.2 Mazingira**

Uharibifu wa mazingira kwa kiasi kikubwa huchangiwa na uwepo wa shughuli mbalimbali za kibinadamu mathalani uvunaji wa mazao ya asili, shughuli za viwanda, kilimo, madini, uvuvi na ufugaji. Shughuli hizi zinapotekelezwa bila kuzingatia athari za mazingira husababisha uharibifu mkubwa wa mazingira. Uhusiano huu wa mazingira na shughuli za kiuchumi huathiriwa na changamoto mbalimbali zikiwemo za mabadiliko ya tabianchi, matumizi mabaya ya rasilimali za asili, uvunaji wa mazao ya asili usiozingatia uhifadhi wa mazingira, matumizi ya mbinu duni za kilimo, uvamizi na uharibifu wa vyanzo vya maji, kupungua kwa rasilimali za asili kama vile maji na mazao ya misitu yakiwemo kuni na mkaa kwa matumizi ya nyumbani na hivyo kusababisha changamoto za afya kwa wazee yakiwemo matatizo kwenye mifumo ya upumuaji na macho makundu ambayo kwa baadhi ya maeneo yamehusishwa na imani za kishirikina na kusababisha vifo kwa baadhi ya wazee.

**Lengo**

Kukuza ushiriki wa wazee katika masuala ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira.

**Matamko ya Sera**

| |
|---|
| Serikali kwa kushirikiana na wadau itafanya yafuatayo:<br>i) Kuhamasisha ushiriki wa wazee katika usimamizi, mipango na mikakati ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi; na<br>ii) Kukuza uelewa kuhusu matumizi ya nishati safi na utunzaji wa mazingira. |

### 3.2.10.3 Virusi Vya Ukimwi (VVU) na Upungufu wa Kinga Mwilini (UKIMWI)

VVU na UKIMWI ni miongoni mwa magonjwa yanayoathiri makundi yote likiwemo kundi la wazee. Kumekuwepo na juhudi mbalimbali ikiwemo kuundwa kwa Kamati ya Uongozi ya SADC kuhusu VVU na UKIMWI (*SADC HIV/AIDS Steering Commitee*) inayoshughulikia masuala ya UKIMWI kwa watu wenye umri kuanzia miaka 50 na kuendelea katika nchi wanachama wa SADC.

Hata hivyo, wazee wamebebeshwa jukumu la kulea wajukuu ambao wazazi wao wamefariki kwa matatizo mbalimbali yakiwemo ya VVU na UKIMWI na maambukizi yanayotokana na uelewa mdogo wa wazee kujikinga na maambukizi. Aidha, baadhi ya wazee hukatisha matumizi ya dawa kwa kukata tamaa ya maisha kutokana na hali ya uzee. Vilevile, kundi la wazee hudhoofika haraka na magonjwa hayo kutokana na kushuka kwa kinga ya mwili.

**Lengo**

Kuhakikisha wazee wanafikiwa na huduma mahsusi za magonjwa VVU na UKIMWI.

**Matamko ya Sera**

| |
|---|
| Serikali kwa kushirikiana na wadau itafanya yafuatayo:<br>(i) Kukuza uelewa kuhusu athari za VVU na UKIMWI kwa wazee; na<br>(ii) Kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji kwa wazee na wanaotumia dawa kutokana na kuambukizwa VVU na UKIMWI hususan wanaoishi vijijini. |

## SURA YA NNE

## MUUNDO WA KISHERIA

Tanzania ina mfumo wa kisheria unaowezesha usimamizi, uratibu na utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Wazee ya mwaka 2003 Toleo la Mwaka 2024. Mfumo huu wa kisheria utatoa msukumo wa utekelezaji na uwajibikaji katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma stahiki kwa wazee. Aidha, usimamizi na utekelezaji wa sheria mbalimbali utachangia katika kurahisisha utekelezaji wa Sera hii. Sheria hizo ni pamoja na: Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii, Sura ya 50 ambayo inatoa fursa kwa wananchi walio katika sekta isiyo rasmi kunufaika na mafao ya uzeeni kupitia uchangiaji wa hiari; Sheria ya Msaada wa Kisheria, Sura ya 21 na Kanuni za Mahakama na Matumizi ya Sheria (Mwenendo wa Mashauri yanayohusisha Makundi ya Walio katika Mazingira hatarishi za mwaka 2019) ambazo zinaelekeza makundi maalum wakiwemo wazee kupata msaada wa kisheria kupitia watoa msaada wa kisheria; Sheria ya Kodi ya Mamlaka ya Serikali za Mtaa, Sura ya 289 ambayo imeweka vigezo kwa wazee kusamehewa kodi za majengo kwa nyumba wanazomiliki na kuishi wao wenyewe pamoja; na Sheria ya Ardhi, Sura ya 113 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji, Sura ya 114 zinahakikisha masuala ya umiliki ardhi yanazingatiwa bila ubaguzi kwa makundi maalum ikiwemo wazee. Hata hivyo, zipo baadhi ya sheria zikiwemo: Sheria ya Mirathi, Sura ya 352 na Tamko la Sheria ya Kimila Na. 4 kupitia Tangazo la Serikali Na. 436 la Mwaka 1963 ambazo zinatambua mila zinazowabagua wazee wanawake hususani katika masuala ya umiliki wa ardhi.

Aidha, Uchambuzi wa Sheria umebainisha kwamba mfumo wa kisheria uliopo hautoshelezi kulinda maslahi mapana ya mzee. Hivyo, kuna Sheria ambazo zitahitaji kufanyiwa marekebisho ili kurahisisha utekelezaji wa Sera

hii na kuwezesha upatikanaji wa huduma stahiki kwa wazee. Sheria hizo ni pamoja na: Sheria ya Msaada wa Kisheria, Sura ya 21 ambayo inahitaji kufanyiwa marekebisho ili kujumuisha bayana masuala mahsusi ya wazee; Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2019 kujumuisha makundi nufaika ya mikopo ya asilimia 10 kutokana na mapato ya Halmashauri ambayo ni wanawake (4%), vijana (4%) na wenye ulemavu (2%). Hata hivyo, sheria hiyo haijatambua kundi la wazee kama kundi maalum linalostahili kupata mikopo hii; na Sheria ya Serikali za Mitaa (Wilaya), Sura ya 287 na Sheria ya Serikali za Mitaa (Miji), Sura ya 288 hazitoi fursa ya uwakilishi maalum wa kundi la wazee kushiriki katika vikao vya maamuzi.

Vilevile, kuna umuhimu wa kuimarisha mfumo wa kisheria utakaolinda na kuendeleza wazee ambao pamoja na mambo mengine utawezesha uwajibikaji wa jamii ikiwemo familia na watoto kuwatunza wazee wao; kuweka usawa wa matunzo kwa wazazi, wazee wanawake na wanaume pamoja na kuimarisha mfumo wa ushirikishwaji wa wazee katika mipango ya maendeleo ngazi mbalimbali.  Hivyo, Sera hii itatoa msingi wa kisheria katika matunzo kwa wazee katika ngazi ya familia, jamii na taasisi.

# SURA YA TANO

# MUUNDO WA KITAASISI

## 5.1 Utangulizi

Mafanikio ya Sera ya Taifa ya Wazee ya mwaka 2003 Toleo la Mwaka 2024, yanategemea muundo wa kitaasisi uliopo ambao unatengeneza uratibu wa uendeshaji, kusimamia utekelezaji, ufuatiliaji na tathimini ili kufikia matokeo tarajiwa. Muundo wa kitaasisi unaainisha majukumu ya msingi kwa taasisi na wadau muhimu ili kufanikisha utekelezaji wa Sera hii. Taasisi zinazohusika ni pamoja na Wizara za kisekta zikiwemo: Wizara yenye dhamana na maendeleo na ustawi wa wazee; Ofisi yenye dhamana na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Wizara yenye dhamana na masuala ya uratibu wa shughuli za Serikali; Wizara yenye dhamana na fedha; Wizara yenye dhamana na mipango; Wizara yenye dhamana na afya, Wizara yenye dhamana na kilimo; Wizara yenye dhamana na mifugo na uvuvi; Wizara yenye dhamana na katiba na sheria; Wizara yenye dhamana ya ujenzi; Wizara yenye dhamana ya uchukuzi; Wizara yenye dhamana na elimu, sayansi na teknolojia; Wizara yenye dhamana na mambo ya ndani ya nchi; na Wizara yenye dhamana na mambo ya nje na ushirikiano wa afrika mashariki. Wadau wengine ni pamoja na: Mashirika ya Kimataifa; Asasi za kiraia; Mabaraza ya Wazee; na Familia. Lengo ni kuhakikisha uwajibikaji wa wadau wote katika kuimarisha utoaji wa huduma kwa wazee.

## 5.2 Majukumu ya wadau

Katika kuimarisha utekelezaji wa Sera hii, Wizara, Idara na Taasisi za Serikali zinazogusa maslahi ya Wazee zitakuwa na majukumu yafuatayo:

### 5.2.1 Wizara yenye Dhamana ya Ustawi na Maendeleo ya Wazee

Wizara itakuwa na jukumu kuu la kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Wazee ya mwaka 2003 Toleo la Mwaka 2024. Majukumu mengine ni pamoja na:

(i) Kuandaa miongozo ya utoaji wa huduma za ustawi kwa wazee katika familia, jamii na kwenye makazi;
(ii) Kusimamia utekelezaji wa mipango na mikakati mbalimbali ya Kitaifa ya kutokomeza ukatili dhidi ya wazee;
(iii) Kuanzisha programu za kuelimisha jamii kuhusu haki, maendeleo na ustawi wa wazee;
(iv) Kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kuwatumia wazee katika utatuzi wa migogoro ya jamii;
(v) Kutoa huduma za msaada wa kisaikolojia na kijamii kwa wazee;
(vi) Kutafuta rasilimali zinazohitajika kuleta ufanisi wa utekelezaji wa Sera;
(vii) Kufanya mapitio ya sheria na ikibidi kuimarisha mfumo wa sheria ili kulinda na kuendeleza ustawi na maslahi ya wazee katika maeneo mbalimbali;
(viii) Kuimarisha mfumo wa kushughulikia vitendo vya ukatili dhidi ya wazee;
(ix) Kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kujiwekea akiba katika mifuko ya Hifadhi ya Jamii; na
(x) Kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa programu zinazohamasisha ustawi na Maendeleo ya wazee nchini.

### 5.2.2 Wizara yenye Dhamana ya Masuala ya Afya

(i) Kuimarisha mfumo wa utoaji wa huduma za afya kwa wazee;
(ii) Kuandaa miongozo ya utoaji wa huduma za afya kwa wazee;

(iii) Kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya afya kwa wazee na jamii nzima;

(iv) Kuandaa mitaala ya kufundishia wataalam wabobezi wa huduma ya afya kwa wazee;

(v) Kuhakikisha utengaji na uendeshaji wa madirisha ya kutolea huduma za afya kwa wazee katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini; na

(vi) Kuhakikisha utekelezaji wa kampeni ya "Mzee Kwanza" katika vituo vya kutolea huduma za afya vya Serikali na binafsi.

### 5.2.3 Wizara yenye Dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

(i) Kuhakikisha Halmashauri zinatekeleza mipango ya utoaji huduma za matunzo, afya na ulinzi kwa wazee;

(ii) Kuwezesha upatikanaji wa rasilimali za kutekeleza programu na mipango ya utoaji huduma ya matunzo kwa wazee kwa ngazi ya Mikoa;

(iii) Kusimamia utekelezaji wa miongozo ya utoaji huduma bora za matunzo na ulinzi kwa wazee katika ngazi ya jamii na kwenye makazi ya wazee;

(iv) Kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa kujiunga na mifuko ya hifadhi ya jamii; na

(v) Kusimamia utendaji wa Mabaraza ya Ushauri ya Wazee kote nchini.

### 5.2.4 Sekretarieti za Mikoa

(i) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera katika Halmashauri za mkoa husika;

(ii) Kuhakikisha Halmashauri zinajumuisha masuala ya wazee katika mipango yake;

(iii) Kuratibu na kusimamia ulinzi na matunzo kwa wazee katika mkoa husika;

(iv) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Sera;

(v) Kuhakikisha upatikanaji wa kanzidata ya wazee katika ngazi za halmashauri zilizo chini ya mikoa husika;

(vi) Kuratibu programu za kuelimisha jamii kujiandaa na maisha ya uzee katika Halmashauri; na

(vii) Kusimamia utendaji wa Mabaraza ya Ushauri ya Wazee katika mkoa husika.

### 5.2.5 Mamlaka za Serikali za Mitaa

(i) Kufanya utambuzi wa wazee na kuainisha mahitaji yao;

(ii) Kuhakikisha upatikanaji wa bima za afya kwa wazee wasiokuwa na uwezo;

(iii) Kuweka mipango ya huduma kwa wazee katika Halmashauri;

(iv) Kuanzisha programu za kuelimisha wananchi kujiwekea akiba katika mifumo rasmi ya hifadhi ya jamii;

(v) Kuratibu na kuimarisha ushirikiano na wadau wanaotoa huduma kwa wazee;

(vi) Kuhamasisha familia na jamii kuwajibika ipasavyo kutoa matunzo na ulinzi kwa wazee;

(vii) Kuwashirikisha wazee katika mipango ya maendeleo ya Halmashauri;

(viii) Kutunga sheria ndogo kwa ajili ya kulinda haki, ustawi na maendeleo kwa wazee;

(ix) Kuandaa programu za kuelimisha jamii kuhusu masuala ya uzee na kuzeeka;

(x) Kuandaa programu za kuelimisha jamii kuhusu mila na desturi zinazokiuka haki na ustawi wa wazee;

(xi) Kuhamasisha na kuratibu wazee kuunda vikundi vya uzalishaji mali na klabu za mazoezi na burudani;

(xii) Kuandaa, kutunza na kuhuisha takwimu za wazee; na

(xiii) Kuwezesha utendaji wa Mabaraza ya Ushauri ya Wazee katika ngazi za Halmashauri hadi kijiji/mtaa.

### 5.2.6 Wizara yenye Dhamana ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

(i) Kuingiza masuala ya maandalizi kabla ya kuzeeka kwenye mitaala ya shule za msingi, sekondari na vyuo; na

(ii) Kuhamasisha matumizi ya teknolojia rafiki ya wazee.

### 5.2.7 Wizara yenye Dhamana ya Usalama wa Raia

(i) Kusimamia masuala ya usalama wa wazee na mali zao katika ngazi zote;

(ii) Kuimarisha upelelezi wa mashauri yanayohusu vitendo vya ukatili na unyanyasaji dhidi ya wazee; na

(iii) Kusimamia na kuimarisha vikundi mbalimbali vya ulinzi shirikishi vya mitaa na vitongoji.

### 5.2.8 Wizara yenye Dhamana ya Fedha

(i) Kuhakikisha Mwongozo wa Bajeti ya Serikali wa kila mwaka unaelekeza ujumuishaji wa masuala ya ulinzi, matunzo na usalama wa wazee;

(ii) Kuwezesha upatikanaji wa rasilimali za kutekeleza programu na mipango ya utoaji huduma ya matunzo kwa wazee;

(iii) Kuhakikisha mafao ya wazee wastaafu yanalipwa kwa wakati; na

(iv) Kuweka vivutio vya kodi ili kuwezesha upatikanaji wa teknolojia wezeshi na vifaa saidizi kwa wazee.

### 5.2.9 Wizara yenye Dhamana ya Masuala ya Mipango

(i) Kuandaa mipango ya maendeleo ya Kitaifa yenye kuzingatia masuala ya wazee; na

(ii) Kuhakikisha masuala ya wazee yanajumuishwa katika mipango ya sekta mbalimbali.

### 5.2.10 Wizara yenye Dhamana ya Masuala ya Hifadhi ya Jamii

(i) Kuboresha na kusimamia utaratibu wa uchangiaji wa hiari katika mifuko ya hifadhi ya jamii, kuzifikia sekta zisizo rasmi kama vile kilimo, uvuvi, ufugaji na biashara;

(ii) Kutoa elimu kwa jamii kuhusu masuala yote yanayohusu hifadhi ya jamii; na

(iii) Kufanya tathmini na utafiti kuhusu hifadhi ya jamii kwa wazee.

### 5.2.11 Wizara yenye Dhamana ya Masuala ya Ujenzi wa Miundombinu

(i) Kuratibu na kusimamia uwepo wa miundombinu rafiki yenye kukidhi mahitaji ya wazee; na

(ii) Kuongeza uelewa kwa jamii kuhusu matumizi sahihi ya miundombinu inayohusu wazee.

### 5.2.12 Wizara yenye Dhamana ya Masuala ya Katiba na Sheria

(i) Kutoa ushauri wa kisheria kuhusu masuala ya wazee; na

(ii) Kusimamia utoaji wa huduma za msaada wa kisheria kwa wazee.

### 5.2.13 Wizara yenye Dhamana ya Masuala ya Kilimo

(i) Kuhamasisha wazee katika matumizi ya teknolojia rahisi za kilimo katika uzalishaji mali; na

(ii) Kutoa elimu ya lishe kwa wazee na uhifadhi wa chakula kwa jamii.

### 5.2.14 Wizara yenye Dhamana ya Mifugo na Uvuvi

(i) Kuhamasisha wazee kutumia teknolojia za kisasa katika ufugaji na uvuvi; na

(ii) Kuelimisha wazee juu ya ufugaji na uvuvi wenye tija.

### 5.2.15 Wizara yenye Dhamana ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki

(i) Kuhakikisha progamu na mipango ya wazee inajumuisha mipango na mikataba ya Kikanda na Kimataifa;

(ii) Kuhamasisha kuridhiwa kwa itifaki na mikataba ya Kikanda na Kimataifa kuhusu ustawi na maendeleo ya wazee; na

(iii) Kuratibu utekelezaji wa itifaki za mikataba ya kimataifa na kikanda na kuratibu uandaaji wa uwasilishaji wa taarifa za mikataba inayohusu wazee.

### 5.2.16 Wizara yenye Dhamana ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari

(i) Kuwajengea uwezo na kuwahamasisha wazee kuhusu matumizi ya teknolojia rahisi; na

(ii) Kuratibu upatikanaji wa mifumo rafiki ya mawasiliano kwa wazee.

### 5.2.17 Wizara yenye Dhamana ya Utamaduni, Sanaa na Michezo

(i) Kuingiza masuala ya waze katika sera na programu za kukuza utamaduni, sanaa na michezo; na

(ii) Kuhakikisha ushiriki jumuishi wa wazee katika michezo na kuimarisha miundombinu ya michezo ili kukidhi mahitaji yao.

### 5.2.18 Wizara yenye Dhamana ya Ujenzi

(i) Kuratibu na kusimamia upatikanaji wa miundombinu rafiki yenye kukidhi mahitaji ya wazee; na

(ii) Kuratibu ushiriki wa wazee kwenye ujenzi wa miundombinu.

**5.2.19 Wizara yenye Dhamana ya Viwanda na Biashara**

(i) Kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa wazee;

(ii) Kubuni na kusambaza teknolojia rahisi na rafiki kwa wazee ili kuongeza tija katika ujasiriamali; na

(iii) Kuanzisha maeneo maalum ya viwanda vidogo kwa ajili ya wazee kuzalisha bidhaa mbalimbali.

**5.2.20 Wizara yenye Dhamana ya Utumishi na Utawala Bora**

(i) Kutoa miongozo inayozingatia watumishi kujiandaa na maisha ya kustaafu mara wanapoajiriwa; na

(ii) Kutoa mafunzo stahiki kwa watumishi wanapokaribia kustafu.

**5.2.21 Wadau wa Maendeleo**

(i) Kutenga na kutoa rasilimali ili kuwezesha utekelezaji wa Sera hii;

(ii) Kushiriki katika shughuli mbalimbali zinazolenga kukuza na kuinua ustawi wa Wazee; na

(iii) Kuwajengea uwezo wadau mbalimbali wanaotekeleza afua za ulinzi na matunzo kwa wazee.

**5.2.22 Asasi za Kiraia**

(i) Kuhamasisha na kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya wazee na kuzeeka; na

(ii) Kutoa ujuzi, utaalam na rasilimali fedha za kutekeleza afua za masuala ya wazee.

**5.2.23 Sekta Binafsi na Taasisi za Dini**

(i) Kuwajengea wazee misingi ya kiimani;

(ii) Kuijengea uwezo jamii kuhusu huduma, ulinzi na matunzo kwa wazee;

(iii) Kushiriki katika ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa afua za ulinzi na matunzo kwa wazee;

(iv) Kutoa huduma stahiki kwa wazee kwa kuzingatia miongozo, kanuni na taratibu za Serikali; na

(v) Kuingiza masuala ya ulinzi na matunzo kwa wazee katika mipango na programu zao.

### 5.2.24 Taasisi za Elimu na Tafiti

(i) Kuratibu na kufanya tafiti kuhusu masuala ya wazee;

(ii) Kutafuta na kutenga rasilimali zinazohitajika kufanya tafiti nakutoa taarifa ya matokeo ya tafiti ili kuwezesha utekelezaji wa Sera hii;

(iii) Kuandaa mafunzo na programu za kutoa elimu kwa jamii kuhusu masuala ya wazee; na

(iv) Kutoa huduma za ushauri elekezi katika masuala ya ustawi wa wazee.

### 5.2.25 Vyombo vya Habari

(i) Kuibua na kutoa taarifa sahihi zinazowahusu wazee kwa wakati; na

(ii) Kuandaa programu za kuelimisha jamii kuhusu maandalizi ya kuelekea uzeeni pamoja na masuala ya haki, matunzo na ulinzi kwa wazee.

### 5.2.26 Mabaraza ya Wazee

(i) Kuhamasisha jamii kuhusu haki, matunzo na ulinzi kwa wazee;

(ii) Kutoa ushauri kwa Serikali katika ngazi mbalimbali kuhusu mipango ya maendeleo na uimarishaji wa huduma kwa wazee;

(iii) Kuwakutanisha wazee ili kujadili masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa;

(iv) Kuelimisha wazee na jamii kuhusu masuala ya uzee na kuzeeka na ushiriki wa wazee katika maendeleo ya Taifa; na

(v) Kuchochea malezi chanya, uzalendo, maadili mema katika jamii na kusaidia katika utatuzi wa migogoro na changamoto mbalimbali katika jamii.

### 5.2.27 Familia na Jamii

(i) Kuhakikisha upatikanaji wa huduma zote za msingi kwa wazee ikiwa ni pamoja na chakula, mavazi, malazi na huduma za afya;

(ii) Kuwalinda wazee dhidi ya vitendo vya unyanyasaji na ukatili wa kimwili, kiakili, kiuchumi, kisaikolojia na kijinsia;

(iii) Kusimamia na kulinda maadili mema katika jamii ili kuhakikisha kuwa wananchi wanazingatia malezi bora; na

(iv) Kutoa taarifa kwenye mamlaka husika juu ya ukiukwaji wa haki za wazee ikiwemo kukosekana kwa matunzo, ukatili na unyanyasaji dhidi ya wazee.

## 5.3 Ufuatiliaji na Tathmini

Ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Wazee ya mwaka 2003, Toleo la Mwaka 2024 utafanywa na Wizara yenye dhamana ya masuala ya wazee. Hata hivyo, ufuatiliaji na tathmini utategemea juhudi za pamoja na ushiriki wa karibu baina ya Wizara mbalimbali, mamlaka za Serikali za Mitaa, mashirika, taasisi za Serikali na zisizo za Serikali pamoja na wadau wa maendeleo na jamii.

Aidha, utekelezaji wa matamko yaliyoainishwa katika Sera utaenda sambamba na Mkakati wa Utekelezaji. Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini umeandaliwa kwenye Mkakati wa Utekelezaji wa Sera. Hivyo, Wizara yenye dhamana na masuala ya wazee itakusanya, kuunganisha na kuchambua taarifa za utekelezaji wa matamko ya Sera. Wadau wote wanawajibika kutoa taarifa stahiki kwa Wizara yenye dhamana ya masuala ya wazee ili kufanikisha jukumu lake la ufuatiliaji na kutathmini maendeleo

na ustawi wa wazee. Wizara yenye dhamana ya masuala ya wazee kwa kushirikiana na wadau wa kisekta itakuwa na jukumu la kuweka viashiria, vigezo na muda wa tathmini.

### 5.4 Hitimisho

Madhumuni ya Sera ya Taifa ya Wazee ya Mwaka 2003 Toleo la Mwaka 2024 ni kutoa mwongozo wa jumla wa utoaji wa haki, ustawi na matunzo kwa wazee ili kuendana na mabadiliko ya ulimwengu hususan katika uchumi, sayansi na teknolojia. Vilevile, Sera hii italiwezesha Taifa hili kufikia lengo la kujali haki, utu, mchango na ustawi wa wazee. Aidha, Sera hii imezingatia ukweli kuwa wajibu wa matunzo na ulinzi kwa wazee ni jukumu la familia na jamii.